# MUONGOZO WA MAJADILIANO

# Pata Pata

Kitabu cha **3**



Kipindi cha
**Watoto**
Redioni Siku
ya Jumamosi

JOHNS HOPKINS BLOOMBERG SCHOOL of PUBLIC HEALTH

Center for Communication Programs

# Muongozo wa Majadiliano

## Kitabu cha 3



Mwongozo huu umefanikiwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID). Johns Hopkins University Centre for Communication Programs itawajibika na matokeo ya kazi hii. Taarifa hii ni maoni ya mtayarishaji si lazima yawakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.

JOHNS HOPKINS BLOOMBERG SCHOOL of PUBLIC HEALTH
Center for Communication Programs



## Yaliyomo

4 Utangulizi
4 Shukrani
6 Namna ya kuanzisha vikundi
11 Mambo ya kuyazingatia wakati wa majadiliano ya vikundi

### Muongozo wa Majadiliano Sehemu ya 1 - 24

14 Sehemu ya 01: Zawadi Kahamia Bwawasugu
16 Sehemu ya 02: Mama Seka na Mpango Mpya
18 Sehemu ya 03: Hogo la Tumaini
22 Sehemu ya 04: Siku ya Ubunifu
24 Sehemu ya 05: Mchezo wa Korosho
26 Sehemu ya 06: Safari ya Shule
28 Sehemu ya 07: Mwanafunzi Mgeni
30 Sehemu ya 08: Baba Kasema
32 Sehemu ya 09: Simu ya Bi Kiduku
34 Sehemu ya 10: Mangi
36 Sehemu ya 11: Kijiji cha Jirani
38 Sehemu ya 12: Siri ya Chandarua
40 Sehemu ya 13: Mzee Limumi
42 Sehemu ya 14: Kinara na Bonye
44 Sehemu ya 15: Chandarua cha Familia ya Bonye
46 Sehemu ya 16: Kishada cha Pipi
48 Sehemu ya 17: Hadithi za Mzee Chanjagaa
50 Sehemu ya 18: Ajali ya Bi Kiduku
52 Sehemu ya 19: Zawadi Mwanasoka
54 Sehemu ya 20: Vipele vya Bi Kiduku
56 Sehemu ya 21: Kazi ya Kujitolea
58 Sehemu ya 22: Bibi Kizee
60 Sehemu ya 23: Mkutano wa Mama Seka
62 Sehemu ya 24: Habari Njema

## Utangulizi

Patapata ni kipindi cha watoto redioni siku ya jumamosi. Kipindi cha Patapata ni mahususi kwa watoto wa shule za msingi wenye umri kati ya miaka 6 mpaka 12. Kipindi hiki kina mada mbalimbali kuhusu mpango wa ugawaji vyandarua mashuleni, kinga ya ugonjwa wa malaria na mada nyingine nyingi za kufurahisha na kuelimisha watoto.

Muongozo wa majadiliano umeandaliwa kwa ajili ya Ajenti wakusaidi kuleta mabadiliko kwenye jamii (CCA). Muongozo wa majadiliano utatumiwa na CCA kuendesha majadiliano ya vikundi sambamba na kipindi cha Patapata.

Mwongozo huu unaelekeza namna ya kuanza kuunda vikundi na kusikiliza kipindi cha watoto redioni. Ili kuhakikisha kama watoto wameelezwa kipindi walichosikiliza, muongozo una maswali ya kuuliza kila mwisho wa kipindi ili kupima uelewa. Na kwenye kila kipindi kuna zoezi kwa ajili ya watoto kufanya kwa pamoja, ujumbe wa kupeleka nyumbani au kazi yakwenda kufanya nyumbani.

Tunatumaini huu mwongozo utawasaidia CCA na vikundi vya watoto kusikiliza, kujifunza na kufurahia kipindi cha Patapata. Tunatumaini kupata maoni yenu juu huu mwongo na kipindi kwa ujumla.

**Kipi kipya:**

Katika muongozo wa majadiliano 3, tumeweka muhtasari wa kila igizo, utakusaidia kulifahamu igizo kama hukulisikia redioni.

Kila baada ya majadiliano na baada ya watoto kutoa mawazo yao, yataje yote kwa ufupi ili kila mtoto ayasikie. Itawasaidia watoto kuelewa na kukumbuka.

## Shukrani:

Baadhi ya sehemu za muongozo huu zimechukuliwa kutoka WHO, CDC, UNESCO na miradi kama Kilimani Sesame, PSI/Tanzania, "Families Matter" Tanzania (T-Marc/AED) "Learning at Toanga Market" Zambia (JHU/CCP), "Straight Talk" Uganda (JHU/CCP) "Ku Saurara!" Nigeria (JHU/CCP), "Soul Buddyz" Afrika ya Kusini (Soul City), "Tools Together Now" (AIDS Alliance), "Child to Child" (TALC/UK) na miradi mingine mingi. Tunapenda kutoa shukrani za dhati vyanzo hivi na makosa yoyote kwenye muongozo ni ya kwetu.

COMMIT inapenda kutoa shukrani kwa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) kwa ushiriki wao kwenye kuandaa kipindi cha watoto redioni. COMMIT inapenda pia kutoa shukrani kwa Maajenti wa kusaidia kuleta mabadiliko kwenye jamii (CCA), shughuli za kupambana na malaria kwenye jamii na kampeni kwenye redio ili kufanya malaria historia Tanzania.



# Namna kuanzisha vikundi vya majadiliano

## A: Mkutano na viongozi wa kijiji

**Kama ilivyo kwenye shughuli zako nyingine, unahitaji ushirikiano kutoka kwa viongozi wa kijiji kwenye shughuli hii pia.**

- o Mweleze kiongozi wa kijiji kuhusu mpango wako wakuunda vikundi vya watoto kusikiliza kipindi cha watoto redioni ili wajifunze kuhusu afya na elimu ya uraia.
- o Muombe akusaidie kutaarifu wazazi wenye watoto wenye umri kati ya miaka 6-12 kwamba, utakuwa unasikiliza kipindi cha watoto redioni kila jumamosi pamoja na vikundi vya watoto kwa kutumia redio yako inayotumia nguvu za mwanga wa jua na baada ya kusikiliza utakuwa unafanya nao majadiliano na mazoezi mbalimbali.
- o Mwabie kiongozi wa kijiji kwamba utakuwa unampa taarifa za maendeleo ya vikundi hivyo.

## B: Mkutano na wazazi

**Ni muhimu sana wazazi waielewe shughuli hii kabla yakuunda vikundi vya watoto kusikiliza kipindi cha watoto. Kwa mfano unaweza**

- o Ukawaomba viongozi wa kijiji watangaze habari ya shughuli hii kwenye mikutano ya kawaida ya kijiji.
- o Muombe mwalimu atangaze habari za shughuli hii kwenye mikutano ya walimu na wazazi.
- o Muombe kiongozi wa dini akuruhusu utangaze habari za shughuli hii kwenye ibada au shughuli nyingine za kidini.
- o Watembelee nyumbani wazazi wa watoto wa umri kati ya 6-12 ili uwape habari za shughuli hii.

**Mfano wa maneno unayoweza kusema kwa kiongozi au mzazi:**

Kama unavyonifahamu, mimi ni Nyonzo bin Kiteto, nafanya kazi ya kujitolea kutoa elimu ya afya kwa jamii. Hivi karibuni kipindi cha watoto kitaanza kusikika redioni kila Jumamosi asubuhi. Ni kipindi cha kufurahisha, kinatoa burudani na elimu juu ya mpango wa ugawaji wa vyandarua shuleni na kinga ya ugonjwa wa malaria kwa watoto wa miaka kati ya 6-12.

Kama moja ya njia ya kuhamasisha afya ya jamii, nitaunda vikundi vya watoto ili wakutane na kusikiliza kipindi cha watoto redioni kila jumamosi. Tutasikiliza kipindi kwa pamoja na kufanya mazoezi au mchezo. Shughuli hii nzima itachukua saa 1.

Kuna wakati nitawapa watoto maswali ili waje kujadili na nyie wazazi au nitawaomba washiriki kwenye shughuli mbalimbali za afya kijijini kwao. Hii ni njia nzuri sana kwa watoto wako kujifunza kwahiyo ushirikiano wako mzazi ni muhimu sana.
Utatoa ruhusa kwa mtoto wako kushiriki kwenye kikundi cha kusikiliza redio?



### C:  Chagua eneo lakusilikizia kipindi cha watoto

Ni muhimu sana uchague eneo kwenye kijiji chako. Eneo ambalo

- o Ni rahisi kufika
- o Lina ukimya wakutosha redio kusikika
- o Lina nafasi ya kutosha watoto wote kuenea na kushiriki michezo

***Hakikisha una ruhusa ya kutumia hili eneo kila jumamosi***

Vikundi vinaweza kusikiliza redio kwenye:

- o Jengo la shule
- o Eneo la shule
- o Kwenye eneo la msikiti au kanisa
- o Chumba cha ofisi ya serikali ya kijiji
- o Chini ya mti ulio kwenye kijiji chenu

### D: Hakikisha shughuli inafurahisha

Waombe watoto watengeneze sheria za kikundi ili kila mtoto apate nafasi ya kuongea, kujifunza na kufurahia.Sheria hizi zinaweza zikawekwa katika maeneo yafuatayo:

1. Wakati kipindi kikiruka redioni
2. Wakati wa majadiliano
3. Wakati wa kufanya mazoezi/maswali
4. Mwisho wa kipindi kuruka
5. Kila baada ya kukutana kusikilza kipindi na kujadili

**Note:** Tumia mifano ifuatayo kama rejea ya sheria unazoweza kutengeneza

*Wakati kipindi kikiruka redioni:*

- Tunawahi kila Jumamosi
- Tunasikiliza kwa kimya ili kila mmoja asikie kipindi
- Tunasikiliza kwa makini tuweze kushiriki kwenye majadiliano

*Wakati wa majadiliano:*

- Tunampa nafasi kila mtu aongee
- Tunaheshimu mawazo ya kila mtu, hata kama hatuyakubali
- Tunafupisha mawazo yote ya muhimu ili kila mtu aelewe

*Wakati wa kufanya mazoezi/maswali:*

- Tunahakikisha kila mmoja wetu anashiriki
- Tunaheshimu mawazo ya kila mtu, hata kama hatuyakubali
- Tunasisitiza pale tunapokubaliana kitu

*Mwisho wa kipindi kuruka:*

- Tunakumbushana yale tunayotakiwa kuyafanya nyumbani (jadiliana na mzazi, fanya shughuli ya nyumbani)
- Tunamshukuru kila mmoja wetu na kukumbushana kuhudhuria kipindi cha wiki ijayo

*Kila baada ya kukutana kusikiliza kipindi na kujadili:*

- Tunajadiliana na wazazi kuhusu tulichojifunza
- Tunafanya shughuli za nyumbani tulizopewa wakati wa majadiliano ya kikundi (mfano: kutembelea nyumba ya jirani kuangalia kama wanachandarua na  wamekitundika)
- Tunajadiliana na watu wengine kuhusu tulichojifunza

Unaweza ukachagua mtoto unayeona anayefaa kuwa kiongozi msaidizi kwa ajili ya kipindi cha kwanza. Halafu wakati wa kipindi hiki waambie watoto hivi, utakuwa unachagua kiongozi msaidizi kwenye kila kikundi. Mtoto atakaye chaguliwa ni yule mtoto atayekuwa mtulivu, anayeshiriki vizuri, mbunifu na mtaratibu.

### E: Toa maendeleo ya shughuli kwa viongozi wa kijiji na wazazi

Baada ya kikundi kukutana mara mbili hadi tatu ili kusikiliza kipindi cha watoto, hakikisha unakutana na viongozi wa vijiji au baadhi ya wazazi ili kuwapa maendeleo ya shughuli hii na kama una swali au unahitaji msaada wao.



# Mambo ya kuyazingatia wakati wa majadiliano ya vikundi

Ili kufanya shughuli yako ya majadiliano na watoto iwe nzuri, kuna mambo kadhaa unatakiwa kuyazingatia. Mambo yenyewe ni haya yafuatayo:

**Jiandae vizuri kabla ya majadiliano;**

- Soma muongozo wa kipindi, maswali yakupima uelewa, ujumbe wa kupeleka nyumbani, kama utahitaji ufafanuzi wa jambo lolote, upate kabla ya majadiliano.
- Hakikisha redio yako ina chaji.
- Waambie watoto wakumbushe kuwahi kusikiliza kipindi.
- Wahi kabla ya watu wengine ili kuhakikisha eneo la kufanyia majadiliano liko katika hali nzuri.

**Toa taarifa kwa viongozi wa kijiji**

Hakikisha unawapa viongozi wa kijiji taarifa za maendeleo au tatizo la vikundi vya majadiliano. Wakati utakapo jenga uzoefu wakuendesha majadiliano, unaweza ukawaalika baadhi wa wazazi au viongozi wa kijiji ili washuhudie majadiliano na Vikundi vya watoto.

***Wape moyo watoto wote washiriki:***

**Wakaribishe washiriki:**

- Hakikisha watoto wote wako huru kwa kuwakaribisha pale wanapofika eneo la shughuli.

**Kusikiliza kwa makini:**

- Hakikisha unatoa nafasi kwa watoto wenye aibu na wakimya na kuwahamasisha watoto wote kushiriki
- Onyesha usikivu kwa watoto kwa kutingisha kichwa, kutabasamu au muangalie mtoto usoni.
- Waulize maswali ili kuonyesha unavutiwa kuwasikiliza (mfano: Kipi unafikiri kilikuwa cha muhimu zaidi?)
- Fupisha majadiliano ili uweze kuangalia uelewa kilichoongelewa na kutoa nafasi ya mrejesho ( mfano: Kama nimeelewa vizuri, umesema hili ni jambo gumu kulifanya?)
- Kama mtoto atatoa jibu amabalo si sahihi, toa nafasi kwa watoto wengine kutoa mawazo ya tofauti badala ya kumrekebisha (Mfano: James, kama nimekuelewa vizuri, umesema malaria inasababishwa na jua, kuna mtu mwenye wazo tofauti na hili?) Hakikisha unataja jibu sahihi mwisho wa majadiliano. (Mfano: Kama Suzana alivyosema, vimelea vya malaria vinaenezwa na mbu na sio maembe au jua kali )

**Maswali ya muhimu:**

- Wakati wote uliza maswali yanayo ruhusu kujieleza,

1. Kwanini?
2. Nini?
3. Wakati gani?
4. Wapi?
5. Nani?
6. Kwa namna gani?

**Angalia tofauti kati ya maswali yafuatayo:**

- Je mmekipenda kipindi tulichokisikiliza?
- Umependa nini kwenye kipindi tulichokisikiliza?

Yapi kati ya maswali yafuatayo ni maswali yaliyoruhusu kujieleza? Maswali yenye kuuliza "kwa nini?", "kwa namna gani?" au Maswali yenye majibu ya ndiyo au hapana?

**Faida ya kuuliza maswali yanayo husu kujieleza:**

- Pindi mtoto anapozungumza na kujibu swali au kutoa maoni, ukimuuliza maswali ya kiudadisi kwa kufuatisha majibu yake hupelekea kufahamu suala kwa kina, kwa kuendelea kuliza, "Sawa, kwahiyo hii ni kwanini?" Kwa mfano mtoto akisema, "Nyumbani kwetu hatupendi kutumia vyandarua" uliza, "Kwanini?" Kama mtoto akisema, "Hatuna sehemu nzuri ya kuvitundika" kisha uliza, "Kuna kitu gani kinawakwamisha kutundika vyandarua?"
- Uliza maswali yanayojitosheleza ili kuhakikisha watoto wanayaelewa. Pia badilisha namna ya uulizaji wa maswali.
- Uliza maswali kuhusu mitazamo ya watu kwa kuwauliza jinsi wanavyohisi/wanavyojisikia na siyo tu mambo wanayoyafahamu. Waombe watoto watoe mifano kwa kila watakachokisema.

**Maswali kwa ajili yako:**

1. Kama watu wakizidi kwenye kikundi chako cha majadiliano, utafanya nini?
2. Kama kila wiki wanakuja watoto wachache, utafanya nini?
3. Utachukua hatua gani kama watoto wa marika mengine wanataka kushiriki (wakubwa au wadogo)?
4. Utafanya nini endapo baadhi ya shughuli zitakuletea matatizo kutoka kwa wazazi?

**Utoaji taarifa**

Mradi wa COMMIT utahitaji kupata taarifa juu ya mambo yanavyokwenda kwenye vikundi vya majadiliano ya Patapata.

Unahitajika kujaza taarifa kila mara unapofanya majadiliano ya Patapata na watoto. Taarifa hizi utaziwasilisha kwa asasi inayokusimamia. Asasi yako ya kijamii nayo itakusanya taarifa hizi nakuziwasilisha makao makuu ya COMMIT kupitia msimamizi wa mradi wa mkoa.

**Taarifa hizi zitatusaidia**

- Kufahamu kama watoto wanafurahia kipindi cha Patapta na kukielewa.
- Watoto wangapi wanasikiliza kipindi na kushiriki kwenye majadiliano ya kikundi.
- Kupata maoni yako ili kuboresha kipindi.



Sehemu ya 01:

# **Zawadi** kahamia **Bwawasugu**

**Bi Kinara, Tumaini na Pipi wanaenda stesheni kuwapokea Maua na Kinara ambao wanarudi nyumbani kutoka shule. Wakiwa stesheni wanakutana na Bila, Tembe na Doto ni watoto wanaosoma shule moja na Tumaini na Pipi. Bi Kinara anashangaa kwanini Bi Kiduku hajafika bado stendi kumpokea Maua. Baadae kidogo wanamuona Bi Kiduku anakuja akipakizwa kwenye baiskeli na Zawadi.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Pipi na Tumaini walikwenda stesheni kufanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Kumpokea Kinara na Maua)
2. Wanafunzi wenzake Pipi walikuwa wanafanya nini pale stesheni?
(***Jibu sahihi:*** Walikua wanacheza na kukimbizana),
3. Bila, Tembe na Doto wanatabia gani?
(***Jibu sahihi:*** Wanatabia ya utundu)
4. Maua anauhusiano gani na Zawadi?
(***Jibu sahihi:*** Ni binamu yake, mtoto wa mjomba wake)
5. Tumaini anapenda kucheza nini?
(***Jibu sahihi:*** Mpira wa miguu)

## Zoezi la 1: Bingili bingili

**Uliza: nani anaweza kuimba wimbo wa:**
*Tuimbe bayoyo, tuimbe bayoyo*
*Joyce aje hapa aonyeshe maringo yake bingilibingili mpaka chini*
*Sisi wote tuko hapa kujifunza bingilibingili mpaka chini*

**Hatua 1:**
**Sema:** sasa tutaunda maneno mengine kwa wimbo huu. Badala ya kuimba kwa kutumia majina yetu halisi, tutajipa majina ya washiriki walio kwenye igizo na tutaimba kwa kutumia majina yetu mapya
**Sema:** Kaeni kwenye mduara.

**Hatua 2:** Wapange watoto kwenye mduara
**Uliza:** *Nani atakua Zawadi? Nani atakua Tembe, Tumaini, Pipi, Bi Kinara, Doto, Maua, Bi Kiduku?*

***Wape nafasi watoto wachague wanapenda kutumia jina gani, kila mtoto achague jina la mshiriki mmoja***

**Sema:** Sasa tutaimba wimbo wa bingilibingili kwa kupiga makofi na kucheza.

***Onyesha mfano jinsi watakavyo piga makofi na kucheza***

**Hatua 3:**
**Sema:** Sasa imbeni wimbo wa bingilibingili kwa tumia majina ya washiriki wa kwenye igizo (Zawadi, Pipi, Tumaini, Tembe, Doto, Maua, Bi Kiduku, Bibi Kinara)

**Mfano:** *Tuimbe bayoyo, tuimbe bayoyo*
*Zawadi aje hapa aonyeshe maringo*
*yake bingili bingili mpaka chini*
*Sisi wote tuko hapa kujifunza bingili bingili mpaka chini*

**Hatua 4:**
**Sema:** Sasa mtafanya zoezi la kuwatambua na kujikumbusha uhusiano wa wahusika wa igizo hili.

**Taja jina moja moja na uliza:**

- Pipi anasoma na akina nani? Taja majina yao?
*(**Jibu sahihi:** Bila, Tembe, Dotto na Tumaini)*
- Kinara na Maua ni rafiki wa kina nani?
*(**Jibu sahihi:** Pipi na Tumaini)*
- Zawadi anakaa dawati moja na nani shuleni?
*(**Jibu sahihi:** Pipi)*
- Bi kiduku ni shangazi yake nani?
*(**Jibu sahihi:** Zawadi)*

## Ujumbe wakufunga kipindi:

Usikose kuja kusikiliza kipindi cha Patapata kila jumamosi nawaalike na wenzako ili tujifunze na kufurahi pamoja. Tutakuwa na michezo mbalimbali wakati wa kujifunza na kujikumbusha yale tutakayojifunza kila tunapokutana.

Sehemu ya 02:

# **Mama Seka** na Mpango Mpya

**Wanafunzi wako uwanjani wanacheza, mara kengele inapigwa na wanaelekea mstarini. Mwalimu mkuu anamkaribisha Mama Seka ambaye anawaeleza wanafunzi juu ya mpango wa ugawaji wa vyandarua shuleni ambao utaanza hivi karibuni. Mama Seka anasisitizia kwa wanafunzi kwamba ni muhimu kufikisha vyandarua hivo salama nyumbani na ni vizuri kuwafahamisha wazazi wao juu ya mpango huo kwani wao ni mabalozi wazuri sana katika kufikisha ujumbe.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Muelimishaji wa malaria alikwenda shuleni kuwapa wanafunzi taarifa gani?
   *(**Jibu sahihi:** Taarifa za mpango mpya wa ugawaji vyandarua bila malipo shuleni)*
2. Kwanini vyandarua vitagawiwa kupitia wanafunzi?
   *(**Jibu sahihi:** Kwa sababu watoto ni mabalozi wazuri sana wa kufikisha ujumbe)*
3. Muelimishaji aliwaambia wanafunzi wakipokea chandarua wanapaswa kupeleka wapi?
   *(**Jibu sahihi:** Wapeleka moja kwa moja nyumbani na wawakabidhi wazazi au walezi)*
4. Ni madarasa gani yatakayo gawiwa vyandarua?
   *(**Jibu sahihi:** 1, 3, 5 na 7 na shule za sekondari kidato cha 2 na 4)*

## Zoezi la 2: Mchezo wa Namba

**Sema:** Leo mtacheza mchezo wa kuhesabu namba, katika mchezo huu mtakaa katika mstari mmoja , na maelezo ya mchezo huo ni haya, hesabu namba 1 mpaka 7, kila mkifika namba 7 anayefuata anaanza tena namba1, mpaka wote muishe. Kila mmoja akukumbuke namba yake.

**Hatua 1:**
**Sema:** Jipangeni mstari mmoja.

**Hatua 2:**
**Sema:** Sasa anzeni kuhesabu namba, (wakati wakihesabu namba kuwa karibu nao ilikuhakikisha wanahesabu kwa usahihi).

**Hatua 3:**
**Sema:** Watajipanga kwenye makundi kama ifuatavyo. Waliosema 1 wanyooshe mkono juu, waambie watoke kwenye mstari na wasimame mkono wako wa kulia, endelea kusema wale waliohesabu namba 3 wanyooshe mkono juu, waambie nao watoke kwenye mstari wasimame mkono wako wa kulia, sema waliohesabu namba 5 na 7 wanyooshe mkono juu na wasimame mkono wako wa kulia pia kuunda kundi moja kubwa la namba 1, 3, 5 na 7.

**Hatua 4:**
**Waambie** wale waliohesabu namba zilizo baki (2, 4 na 6) wote kwa pamoja wataunda kundi moja, wasimame mkono wako wa kushoto.





**Hatua 5:**
**Waulize** kama kila kundi linakumbuka namba yake anza na kundi la kwanza, ambalo ni namba 1, 3, 5 na 7 na kundi la pili lililoko mkono wa kushoto lenye namba 2, 4 na 6.

**Hatua 6:**
**Sema:** Sasa walio kundi la mkono wako wa kulia nisawa na darasa la1, 3, 5 na 7.

**Hatua 7:**
**Sema:** Kunampango wa ugawaji wa vyandarua bila malipo mashuleni utakaofanyika kila shule hivi karibuni. Ushirikiano wenu unahitajika sana wanafunzi. Serikali imeamua kutumia njia hii mpya ya kugawa vyandarua kupitia ninyi wanafunzi kwa sababu ninyi ni mabalozi wazuri sana wa kufikisha ujumbe.

Ukipokea chandarua chako unatakiwa ukipeleke moja kwa moja nyumbani kwenu na kuwakabidhi wazazi au walezi wako.

**Sema:** Sasa katika mpango wa ugawaji vyandarua shule ni darasa 1, 3, 5 na 7 tu ndio watakaogawiwavyandarua. Kwa mchezo huo ni kundi moja tu la mkono wakulia ndio watakaogawiwa vyandarua. Kundi lililo baki ni madarasa ambayo hayatagawiwa vyandarua, madarasa haya ni la 2, 4 na 6.

**Hatua 8:**
**Sema:** Zeozi hili liwasaidie kukumbuka madarasa yanayohusika, msaidie kuwajulisha wanafunzi wote walio katika madarasa hayo, Ili siku ya kuandikishwa wawe shuleni, na siku ya kugawa vyandarua wawepo pia ili wapokee vyandarua vyao.

**Hatua 9:**
**Uliza:** Kama wameelewa au kama kuna mwenye swali kuhusu mpango wa ugawaji vyandarua shuleni. Waambie sasa wakae mkao wao wa kawaida.

**Hatua 10:**
**Himiza:** Kuwa mpango huu utatumia wanafunzi kama mawakala wa kufikisha vyandarua nyumbani na katika jamii. Mpango huu utahusisha pia shule za sekondari kidato cha 2 na 4.

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

**Kwanza:** Mkirudi nyumbani muwaambie wazazi, walezi, marafiki na majirani zenu kuhusu mpango wa kugawa vyandarua shuleni.

**Pili:** Wafikishieni taarifa wanafunzi wote walio katika madarasa yatakayogawiwa vyandarua.

Sehemu ya 03:

# Hogo la Tumaini

**Zawadi na Pipi wanaenda hospitali kumwaangalia Tumaini ambaye aliumia mguu alipokuwa anacheza mpira shuleni. Anaporudi nyumbani, Zawadi anamuelezea Bi Kiduku kuhusu mpango wa ugawaji wa vyandarua shuleni ambao utaanza hivi karibuni na madarasa yatakayohusika ni darasa la 1, 3, 5, 7 na kidato cha 2 na 4. Zawadi pia anamuelezea watakao kosa mwaka huu watapatiwa mwakani.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Kwanini Tumaini alilazwa hospitali?
   *(**Jibu sahihi:** Kwasababu aliteguka mguu akawekewa hogo)*
2. Kwa nini Tumaini analala kitanda kimoja na Bonye?
   *(**Jibu sahihi:** Kwasababu walikuwa na chandarua kimoja tu)*
3. Zawadi alisema ni kwanini madarasa machache yatagawiwa vyandarua?
   *(**Jibu sahihi:** Kwasababu vyandarua hivi ni vyakuongezea tu vile ambavyo vimepungua, kwa kuchakaa au kuchanika)*
4. Maua alisema ni madarasa gani yatakayo gawiwa vyandarua?
   *(**Jibu sahihi:** 1, 3, 5 na 7 na kidato 2 na 4)*

## Zoezi la 3: Chemsha Bongo

### Utangulizi wa zoezi:

**Uliza maswali ya kufuatilia zoezi lililopita**

- Waulize kama waliwaeleza wazazi au walezi wao kuhusu mpango wa ugawaji vyandarua shuleni, waliofanya hivyo wanyooshe mikono juu, angalia kama ni idadi kubwa ya washiriki imefikisha ujumbe wa mpango wakugawa vyandarua shuleni?
- Dodosa, ni kwa nini wale ambao hawakunyoosha mkono hawakuweza kufikisha ujumbe kwa wazazi au walezi wao?
- Wapongeze waliofikisha ujumbe, na himiza wale ambao hawakufikisha ujumbe kwa wazazi wafanye hivyo na waambie utataka kujua kama wameweza kufikisha ujumbe mtakapo kutana tena jumamosi ijayo.

Wambie zoezi la leo litakuwa ni chemsha bongo na kutakuwa na zawadi kwa timu itakayoshinda.

**Hatua 1:**
Wagawe washiriki katika timu mbili, kila timu ichague jina lake.

**Hatua 2:**
Andaa karatasi ya kuandika matokeo, igawe katika pande mbili andika majina ya timu zao moja kila upande. kila timu itakapo jibu swali kwa usahihi wape alama 30 na kama watakosa weka sifuri au deshi.

**Hatua 3:**
**Sema:** Nitauliza swali kwa timu zote, timu iliyotayari kujibu itanyoosha mkono, itakayonyoosha ya kwanza itapewa nafasi ya kwanza kujibu

Toa nafasi ya kujibu swali, waambie nafasi ni kutoa jibu moja kama watakosa uliza swali hilo hilo timu ya pili, iwapo nao watakosa, weka alama ya sifuri au deshi kwa pande zote, kisha wape jibu sahihi kabla ya kuwauliza swali lingine.

Sisitiza kuwa mchezo huo ni chemsha bongo, hivyo wanatakiwa kutoa majibu kwa haraka. Ruhusu washiriki wa kila timu kusaidiana kutoa jibu sahihi ndani ya muda uliowapa.

**Hatua: 4:**
Wape muda wa kujibu swali moja mfano, dakika 1, Kama hakuna timu iliyonyoosha mkono weka sifuri kwa kila timu halafu wape jibu sahihi.

**Hatua 4:**
Endelea kuuliza maswali kwa utaratibu huu mpaka yote yaishe

**Hatua 5:**
Kwa pamoja na washiriki jumlisha alama za kila timu ili kubaini mshindi

***Ipongeze timu iliyoshinda, kama una zawadi wape zawadi.***

**Hatua 6:**
**Waonyeshe watoto picha namba 1 na 2 huku unawauliza maswali yafuatayo**

**Uliza:** Kwa nini vyandarua vinatolewa kwa jamii kupitia watoto wa shule?
(***Jibu sahihi:*** Watoto wa shule watagawiwa vyandarua kwa sababu wao ni mawakala wa zuri wakufikisha ujumbe nyumbani ).

**Uliza:** Kwanini vyandarua vitagawiwa kwa baadhi ya madarasa tu?
(***Jibu sahihi:*** Vyandarua vitagawiwa kwa baadhi ya madarasa kwasababu vyandarua hivi ni vyakuongezea tu vile ambavyo vimepungua, kwa kuchakaa au kuchanika)

**Uliza:** Itakuaje kuhusu wanafunzi watakaokosa vyandarua mwaka huu?
(***Jibu sahihi:*** Wanafunzi watakao kosa mwaka huu watapata mwakani)

**1**




**2**



## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Madarasa 1, 3, 5 na 7 tu ndiyo yatakayopewa vyandarua ili kuongezea vyandarua vilivyopungua kwa kuchakaa au kuchanika.

Picha namba 1




Picha namba 2



Sehemu ya 04:

# **Siku** ya **ubunifu**

**Mwalimu Chewa anawapa zoezi wanafunzi wake wafikirie na kubuni ni nini wanataka kuwa baadae na kisha waje kuonyesha darasani. Wanafunzi wanaanza kuonyesha ubunifu wao. Kuna daktari, mjasiriamali, mwana mazingira na muimbaji. Zawadi anaonyesha kitu cha ubunifu kwa kutengeneza redio na kisha nyimbo ya Patapata inasikika, wanafunzi wanafurahi sana.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Tembe alimjibu nini mwalimu kuhusu sababu yakwenda kusoma
   (***Jibu sahihi:*** Tembe alijibu wanansoma ili kuondoa ujinga)
2. Bila alisema anataka kuwa nani?
   (***Jibu sahihi:*** Supastaa)
3. Mwalimu Chewa alisema Pipi anaweza kuja kuwa nani?
   (***Jibu sahihi:*** Atakua mtaalam wa mazingira)
4. Nani alisema anataka kuwa mwanasayansi na alitengeneza ni?
   (***Jibu sahihi:*** Zawadi alisema anataka kua mwanasanya na alitengeneza redio)

## Zoezi la 4: Matarajio na wajibu

**Sema:**

1. Zoezi linalofuata ni la kusalimiana, ambapo watajenga kufahamiana zaidi miongoni mwao Kwa kuchanganyika huku wakiongea, waambie maongezi yao yataongozwa na maswali utakayo wasomea. Soma swali moja la kwanza kama mfano usalimiane na mtoto mmoja kwa kuunda sentensi inayo jibu swali la kwanza.
2. Sema swali la kwanza la kufahamiana ni "unatarajia wazazi wafanye nini ili kukukinga na malaria?" waambie sentensi ya kila mmoja itaanza" mimi natarajia wazazi wangu wa……… ili wanikinge na malaria. Hapo kwenye dashi ajaze kile anachotarajia wazazi wake wafanye ili kumkinga na malaria.
3. Uliza kama wameelewa wanachotakiwa kuongea

**Sasa wagawe washiriki katika miduara miwili, wa nje na wa ndani**



**Hatua 1:**
Hakikisha kila mmoja ana mwenzake atakaye salimiana nae

**Hatua 2:**
**Sema:** Mtaanza kusalimiana huku mshikana mikono ya kulia, na kuulizana majina, na darasa analo soma.

**Hatua 3:**
**Sema:** Aliye mduara wa nje amuulize mwenzake swali la kwanza kama lilivyo hapo juu "unatarajia wazazi wafanye nini ili kukukinga na malaria?"

**Hatua 4:**
**Sema:** Aliye mduara wa ndani ataanza kujibu kwa kukamilisha sentensi hii mimi natarajia wazazi wangu wa………........................................ ili wanikinge na malaria.

**Hatua 5:**
**Sema:** Aliye mduara wa ndani naye sasa amuulizea mwenzake wa mduara wa nje swali lile lile naye atajibu kwa kukamilisha sentensi ile ile , waambie pale kwenye dashi kila mmoja anatakiwa kutaja matarajio yake kwa wazazi wake.

**Hatua 6:**
**Sema:** Peaneni mikono ya kuagana, Baada ya hapo mtaachana.

**Hatua 7:**
**Sema:** Kila mmoja aliye mduara wa ndani anasogea hatua mbili kulia kwake.

**Hatua 8:**
**Sema:** Mtu aliye wa tatu toka alipokuwa upande wa kulia ndiye atakaye kuwa mwenzake kwa swali la pili.

**Hatua 9:**
**Sema:** Mlio mduara wa ndani ndio mtakuwa wa kwanza kuuliza swali. Ila wanzeni kwa kusalimiana, kutaja majina na darasa analosoma. Swali la maongezi ni "Je, wewe unatakiwa kufanya nini ili kujikinga na malaria?"

**Hatua 10:**
**Sema:** Aliye mduara wa nje ataanza kujibu kwa kukamilisha sentensi hii mimi natakiwa ku ….................................….. ili nijikinge na malaria. Sema mtafanya kama swali la kwanza, aliye nje atauliza swali na aliye mduara wa ndani atajibu kwa kukamilisha sentensi kama yule mwenzake alivyofanya.

**Hatua 11:**
**Sema:** Sasa mtazunguka vyovyote wanavyotaka ili mradi kila mmoja aweze kusalimiana na yeyote kwa kuuliza jina na darasa analosoma tu. Fanyeni hivyo kwa watu wawili.

**Hatua 12:**
**Sema:** Sasa mkae katika mduara mmoja. Kwa kukamilisha zoezi, uliza nani anakumbuka mtu wa mwisho kusalimiana nae? Amtaje kwa jina na darasa analo soma.

**Hatua 13:**
**Uliza:** Nani anakumbuka matarajio ya mwenzeke toka kwa wazazi wake aliyomwambia?

**Waambie wajipigie makofi matatu makubwa kwa kujipongeza kufanikisha mchezo huo**

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Ili kuweza kujikinga na malaria unatakiwa kuzungumza na wazazi wako kuhusu umuhimu wa kila mtu kwenye familia kulala kwenye chandarua kila usiku.

Sehemu ya 05:

# Mchezo wa Korosho

**Ni msimu wa korosho kijijini, Zawadi na wenzake wanapata korosho nyingi sana. Tembe na Doto wanawafundisha akina Zawadi mchezo uitwao sago, katika mchezo huo Pipi ndo anakuwa mshindi. Bila anawashauri akina Tembe wakauze korosho walizopata kwa Mangi ili wapate hela ya kutumia njiani katika safari yao ya shule.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Bila, Tembe na Doto walimuuzia nani korosho zao?
(***Jibu sahihi:*** Mangi)
2. Kwa nini mwalimu alimwambia Mangi hawezi kugawiwa chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Kwasababu mpango huu unagawa vyandarua kwenye jamii kupitia wanafunzi shuleni)
3. Mwalimu alisema wanafunzi wanatakiwa kufanya nini ili wagawiwe vyandarua?
(***Jibu sahihi:*** Wanafunzi wanatakiwa kuandikishwa majina kwa mwalimu wa darasa)
4. Mwalimu alisema mtoto wa Mangi aliye darasa la pili atapata lini chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Atapata chandarua mwakani atakapo ingia darasa la 3)

## Zoezi la 5: Simu

### Maelekezo ya zoezi

1. Watoto wote wakae katika mstari mmoja ulionyooka.
2. Waeleze watoto kwamba utasoma ujumbe kwa sauti nawao warudie kusema huo ujumbe kwa sauti kubwa

   **Soma huu ujumbe kwa watoto**

   *" Vyandarua vitagawiwa kila mwaka kwa darasa la 1, 3, 5 na 7"*

**Baada ya watoto kusema huu ujumbe hapo juu kwa sauti**

3. Waeleze watoto kwamba utamnong'oneza mtoto aliye mwanzo wa mstari, na mtoto huyo amnong'oneze huo ujumbe mtoto anayefuata, mpaka wote watakapo maliza kunong'onezana. Ujumbe utakao mnong'oneza mtoto wa kwanza kwenye sikio ni "watoto watakaogawiwa vyandarua wataandikishwa darasani kwao na walimu wao wa darasa, nao niwa darasa la 1, 3, 5 na 7."
4. Baada ya watoto kumaliza kunong'onezana, wa katikati na mwisho watatakiwa kueleza walichonong'onezwa na wenzao kwa sauti ya juu kwa kundi zima.

(**Angalizo:** ujumbe watakaosema unaweza kuwa tofauti na ule wa mwanzo lakini usiwaeleze watoto wakati huo)

5. Baada ya watoto kusema walichonong'onezwa wenzao utatakiwa kurudia maelezo kama yalivyokuwa awali kwa kundi zima ili wasikie. Waulize watoto kama maelezo mawili ya mwisho yalikuwa sawasawa naya kwanza.
6. Waulize maswali yafuatayo:
**Uliza**: Kwa nini unadhani maelezo ya mwisho yanatofautiana na yale ya mwanzo? (au kama haikubadilika, kwa nini?)

(**Angalizo:** Sababu zinaweza kupelekea ujumbe kubadilika ni kama zifuatazo: kulikuwa na taarifa nyingi, sentensi ilikuwa ndefu sana, kila mtu alitakiwa kurudia alichosikia kwa mtu aliyekuwa anamfuatia, kwa hiyo kila mtu alipokosea, iliongezeka kwenye makosa ambayo mtu aliyetangulia alikuwa ameyafanya kwa kurudia sentensi)

## Ujumbe wa kuhitimishia kipindi

**Kwanza:** Wanafunzi katika madarasa yaliyochanguliwa wanapaswa kuwepo shuleni kipindi cha uandikishwaji majina

**Pili:** Wanafunzi wanatakiwa kueleza majina yao kamili kwa walimu wa darasa wakati wa uandikishwaji

Sehemu ya 06:

# Safari ya Shule

**Wanafunzi wako shuleni wanasubiri kupanda basi kuaanza safari yao. Mwalimu Sango anagundua Bila hakutoa mchango wa safari,kwahiyo anamshusha na basi linamuacha.Mwalimu Sango anamuonea huruma na kulisimamisha basi ili Bila aweze kupanda. Lakini Bila anatumia hela yote kulipia safari na kuwaacha Tembe na Dotto bila hela yoyote ya kutumia katika safari.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi

1. Mwalimu gani alikwenda na wanafunzi pikiniki?
   (***Jibu sahihi:*** Mwalimu Sango)
2. Mwalimu aliwaambia ni utaratibu gani utatumika kuingia kwenye gari?
   (***Jibu sahihi:*** watainigia mmoja mmoja na atakuwa anawaita majina)
3. Kwa nini jina la Bila halikuwepo kwenye orodha?
   (***Jibu sahihi:*** kwa kuwa hakuwa amelipa hela)
4. Mwalimu aliuliza vyandarua vitagawiwa wapi?
   (***Jibu sahihi:*** Darasani)
5. Na kabla ya kugawiwa vyandarua wanafunzi watafanya nini?
   (***Jibu sahihi:*** Watajiandikisha kwa mwalimu wa darasa)

## Zoezi la 6: Igizo

1 **Sema:** watoto wanne wajitolee, mmoja ataigiza kuwa mwalimu, na watatu ni wanafunzi ambao watakuwa hawakujiandikisha. Waliobaki wote watakuwa wanafunzi waliojiandikisha.

2 **Sema:** anayeigiza nafasi ya mwalimu, asimame mbele yao na wale wengine wote waliojiandikisha wakae pamoja karibu na mwalimu.

3 **Sema:** wale watatu ambao hawakujiandikisha watakaa mbali na wenzao wawe wanacheza.

4 **Sema:** mwalimu atakuwa anawagusa mmoja baada ya mwingine wale walio karibu nae. Kule kuwa gusa ndio kuita majina kwa wale walio jiandikisha.

5 **Sema:** wale watatu wanaona zoezi lile la kuguswa wenzao nao wanakuja mbio ila wanakuta zoezi la kuguswa limekwisha. Hii ina maana majina yao hayapo kwenye orodha.

6 Wanajaribu kuwa sogelea wenzao, lakini mwalimu hawagusi, wanauliza kwa nini anawabagua?( wafanye kwa vitendo bila kusema) Mwalimu nae anawauliza wakati anawagusa wenzao walikuwa wapi?( nae aonyeshe kwa vitendo bila kusema) waonyeshe kwa vitendo kuwa walikuwa wanacheza. Hii ina maana wakati wenzao wanajiandikisha hawakuwepo darasani, hivyo hawakuandikishwa.

7 Sasa wale watatu waonyeshe kuomba msamaha, kwa vitendo wainame kwa kumuelekea mwalimu, na mwalimu aonyeshe kwa vitendo kukubali kuwasamehe na kuwaweka pamoja na wenzao ikiwa ni pamoja na kuwagusa kama alivyowagusa wale wengine mwanzo. Ulizani siku ngapi zimetengwa kwa ajili ya kujiandikisha?
(***Jibu sahihi:*** siku moja)

8 **Sema:** Hii ina maana kwamba wanafunzi wa madarasa yatakayogawiwa vyandarua wahakikishe wako darasani siku ya kujiandikisha, usikose ni siku moja tu. Usipo jiandikisha hutapata chandarua.

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Wanafunzi wa darasa la 1, 3, 5, 7, kidato cha 2 na 4 ndio watakaogawiwa vyandarua. Kama unasoma katika madarasa haya, hakikisha unakuwepo darasani siku ya kujiandikisha ili upate chandarua.

Sehemu ya 07:

# **Mwanafunzi** mgeni

**Ni siku ya kwanza Bonye kwenda shuleni tangu alipoanza kuishi kwa akina Tumaini. Anakutana na akina Bila ambao wananza kumchokoza na kumtania. Bonye anamueleza mwalimu kuwa hakuwepo siku aliyokuwa anaandikisha wanafunzi wenzake kwani alikuwa bado hajaamia shuleni hapo.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi

1. Mwanafunzi mpya jina lake ni nani?
   (***Jibu sahihi:*** Bonye au Tumbotukile)
2. Bonye alimfanya nini Bila?
   (***Jibu sahihi:*** Alimgonga kwa bahati mbaya)
3. Mwalimu alisema nini baada ya kuingia darasani?
   (***Jibu sahihi:*** Anaona sura ngeni darasani)
4. Mwalimu alimwambia nini Bonye?
   (***Jibu sahihi:*** Amtajie jina lake kamili, na utaratibu wa kumpatia chandarua siku nyingine)
5. Mwalimu alisema ugawaji wa vyandarua utafanywa kwa siku ngapi?
   (***Jibu sahihi:*** Tatu)

## Zoezi la 7: Alama ya pata na chandarua

Kwanza waonyeshe watoto picha namba **3** halafu soma maswali yaliyo chini ya picha

1) Unaona nini kwenye jina la Bahati na Chava?
   (***Jibu sahihi:*** Alama ya pata na chandarua mbele yake)
2) Uliza nini maana ya alama ya pata na chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Wamejiandikisha na watapata chandarua)
3) Uliza kwenye jina la Kadenge una ona nini?
   (***Jibu sahihi:*** Alama ya kosa na hakuna chandarua)
4) Uliza kwa nini jina la Kadenge lina alama ya kosa na hakuna chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Hakujiandikisha na hatapata chandarua)
5) Utamshauri Kadenge afanye nini ilipate chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Amtaarifu mwalimu wake wa darasa, atamuandikisha na atapata chandarua baadae)


## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Himiza kuwa siku ya kuandikishwa na mwalimu darasani ni moja tu, hivyo ambaye hatajiandikisha amtaarifu mwalimu wake wa darasa ili aweze kuandikishwa.

**Muhimu:** Mkumbushe rafiki/mwanafunzi mwenzako ambaye hajaandikishwa afanye hivyo kwa kuwa vyandarua vitatolewa kwa wanafunzi walioandikisha tu.



## Picha namba 3



Sehemu ya 08:

# **Baba** kasema

**Zawadi, Pipi na Tumaini wako kibarazani wanacheza huku wakimsubiri Maua aje na redio wasikilize kipindi cha Patapata. Baada ya kusikiliza kipindi hicho, watoto wanaanza kuulizana maswali kuhusu ujumbe wa kipindi kwa siku hiyo. Zawadi na Tumaini wanatoa wazo zuri ambao wengine wanalifurahia.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Kina Zawadi walikuwa wanacheza mchezo gani?
   *(Jibu sahihi:* Baba kasema tuchoreee)
2. Pipi alisema mama kasema tuchore nini?
   *(Jibu sahihi:* Mbu)
3. Kinara alieleza mbu yukoje?
   *(Jibu sahihi:* Ana kichwa, kifua na tumbo, ana mabawa mawili… miguu sita, na ana mrija wa kunyonyea damu)
4. Tumaini na Zawadi walitoa wazo gani?
   *(Jibu sahihi:* Waanze kukaa pamoja na kusiliza Patapata na siku nyingine wamualike Mama Seka)

## Zoezi la 8: Igizo la kikundi cha patapata

**Hatua 1:**
Waambie mtoto mmoja ajitolee kuwa redio.Atakaa chini katikati ya wenzake

**Hatua 2:**
**Sema:** mwingine ajitolee kuwa mtoa  elimu ya malaria, naye akae karibu na radio.

**Hatua 3:**
Waliobaki baadhi watakuwa watoto wanaosikiliza kipindi cha Patapata. Hao washikane mikono na wazunguke redio na CCA na wakae chini.

**Hatua 4:**
**Sema:** Mkiwa katika mduara wote muangalie mmoja wa wale wawili walio katikati yenu ambae ni redio,  hii inaonyesha mnasikiliza redio.

**Hatua 5:**
**Sema:** Mtoto mwingine aliye ndani ya mduara ambae nimtoa elimu ya malaria, awafundishe wenzake namna ya kuchomeka chandarua.

**Hatua 6:**
Watoto wengine watatu wawe nje, pembeni kabisa ya mduara, wawe wamesimama mbalimbali bila kushikana mikono, waambie hao hawajajiunga na kikundi cha kusikiliza Patapata. Ndio maana wako mbali na hawajashikana mikono.

**Hatua 7:**
Sasa mmoja wao hao walio nje ya mduara awe amejiinamia na ni mnyonge.

**Hatua 8:**
**Sema:** Huyu mtoto mnyonge ana mawazo na maswali mengi kuhusu malaria, lakini hana mtu wa kumuuliza. Kwa kuwa mikono yake haina mtu wakumshika.

**Hatua 9:**
**Sema:** Kukaa chini nakushikana mikono ni kujadiliana na kubadilishana elimu juu ya malaria huku mkisaidiwa na mtoa elimu wa malaria, na kipindi cha patapata redioni. Ndio maana redio na mtoa elimu wa malaria wako katikati yenu.

**Hatua 10:**
**Uliza:** kama kuna mwenye swali.

**Sema:** wale wenye uwezo wa kupata redio nyumbani au shuleni wanaweza kuunda vikundi vidogo vidogo (vya watu 10) ili kusikiliza na kujadiliana kuhusu umuhimu wa kulala kwenye chandarua.

Baada ya maswali waambie washiriki wasimame kwenye duara, wapige makofi wakiimba wimbo wa sauti ya vijana msilale, lale, lale.. (Wataongeza maneno yafuatayo: umoja ni nguvu, tushiriki pamoja tutokomeze malaria.)

***1. Kiongozi:***
*Watoto msilale, lale, lale, lale*
*Watoto msilale bado mapambano*
*Wote: Nasisi hatulali, lali, lali*
*Nasisi hatulali*
*Bado mapambano.*

***2.Kiongozi:***
*Umoja ndio nguvu, nguvu, nguvu*
*Umoja ndio nguvu bado mapambano.*
*Wote: Tushiriki pamoja moja moja*
*Tushiriki pamoja*
*Tutokomeze malaria.*

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Hata kama mtoa elimu wa malaria hayupo karibu, watoto mnaweza kutafuta redio na kusikiliza Patapata kwa pamoja. Shiriki kikamilifu kusikiliza Patapata na kujadiliana na wenzako ili kuelewa zaidi namna yakutokomeza ugonjwa wa malaria.

Sehemu ya 09:

# Simu ya **Bi Kiduku**

**Maua na Zawadi wanamsindikiza Bi Kiduku dukani kwa muuza simu. Wakiwa dukani wanakutana na Mwalimu Chewa ambaye anamkumbusha Zawadi kuwa siku ya kugawa vyandarua imekaribia kwahiyo asisahau kuwepo darasani siku hiyo.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Bi Kiduku alitaka akina Zawadi na Maua wamsindikize wapi?
   ***(Jibu sahihi:*** Dukani)
2. Bi Kiduku alitaka kununua nini dukani?
   ***(Jibu sahihi:*** Simu inayoitwa hedifoni)
3. Zawadi alimwambia shangazi yake hedifone nini?
   ***(Jibu sahihi:*** Hedifoni ni spika za kuweka masikioni)
4. Kwa nini Mwalimu Chewa alisisitiza Zawadi awepo darasani wiki ijayo?
   ***(Jibu sahihi:*** Kwa kuwa watagawiwa vyandarua)
5. Bi Kiduku alimwambia nini mwalimu Chewa kuhusu mpango wa vyandarua shuleni?
   ***(Jibu sahihi:*** Kuwa anaujua na anasuburi chandarua nyumbani).

## Zoezi la 9: Kusoma chati pindu

Waonyeshe watoto picha namba **4** halafu sema:

Mtoto mmoja ajitolee kusoma sentensi moja moja kwa sauti. Nyoosha mkono nikuchague.

Watoto wakimaliza kusoma uliza maswali yafuatayo ili kuhakisha kama wameelewa ujumbe kwenye bango.

**Uliza:** Vyandaura vitagawiwa wapi?
(***Jibu sahihi:*** Vitagawiwa darasani)
**Uliza:** Baada ya kupokea chandarua mwanafunzi anatakiwa kufanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Anatakiwa kuweka sahihi, na kapeleka chandarua nyumbani na kuwakabidhi wazazi au walezi).

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Hakikisha unakuwepo darasani siku ya kugawa vyandarua ili upate chandarua chako na kukipeleka nyumbani.

Picha namba 4

# MPANGO WAKUGAWA VYANDARUA SHULENI

- Vyandarua vitatolewa darasani
- Walioandikisha tu ndio watakaopewa chandarua.
- Hakikisha umewaka sahihi baada ya kupokea chandarua
- Peleka chandarua nyumbani.
- Wakabidhi wazazi chandarua.

Sehemu ya 10:

# Mangi

**Wanafunzi wanagaiwa vyandarua iliwapeleke nyumbani. Zawadi, Pipi na Tumaini wanakutana na Mangi ambaye anawaomba wamuuzie vyandarua ili aweke dukani kwake, ila wao wanakataa. Baadae kidogo Bila anataka kumnyang'anya Tumaini chandarua chake, Mangi anarudi na kumsaidia Tumaini. Bila anaondoka bila chandarua huku akilalamika.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Mwalimu alisema wanafunzi wapeleke wapi chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Nyumbani)
2. Kwanini Tumaini alitaka kuficha chandarua chake kwenye begi?
   (***Jibu sahihi:*** Alikuwa ataki Bila amsubue)
3. Mangi aliwaambia nini kina Zawadi?
   (***Jibu sahihi:*** Wamuuzie chandarua aweke dukani)
4. Pipi alisemaje kuhusu vyandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Wakilala kwenye chandarua watawakinga majirani na jamii nzima)
5. Bila alikuwa anamyang'anya nani chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Tumaini)

## Zoezi la 10: Kusoma picha

**Waonyeshe watoto picha ya namba 5 kwenye ukurasa unaofuata, halafu soma maneno yaliyo chini ya picha,**

1 **Sema**, angalieni hii picha kwa makini. Kwa ajili ya majadiliano, mtaanza na picha **A**, ikifuatiwa na **B** na mwisho picha **C**
2 Waonyeshe picha **A**, uliza kama kila mmoja ameiona vizuri?
3 **Uliza** je unaona nini?
(***Jibu sahihi:*** Mwalimu akimkabidhi mwanafunzi chandarua)
4 Sasa waambie wangalie picha **B**, onyesha picha hiyo kwa kundi
5 Mzazi anafanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Mzazi anapokea chandurua)
6 Unapaswa kufanya nini mara wapatapo chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Baada ya kupata chandarua, unakipeleke nyumbani na kukikabidhi wazazi/walezi wako)
7 Waambie picha inayofuata ni **C**, ionyeshe kwa kundi.
8 **Uliza** mzazi nafanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Anamkabidhi jirani chandarua)
9 Waonyeshe tena ile picha **C**,
10 Kwanini mzazi anampa jirani chandarua?
(***Jibu sahihi:*** kwasababu anavyo vya kutosha, kile ni cha ziada)

**A** **B** **C**




## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Kama nyumbani vipo vyandarua vya kutosha, mkumbushe mzazi au mlezi ampe jirani ambae hana chandarua.Ukimkinga jirani na malaria unajikinga na wewe.

**Picha namba 5**

**A** **B** **C**



## Sehemu ya 11:
# **Kijiji** cha **Jirani**

**Kinara na Maua wako safarini wanaelekea kijiji cha jirani kuwatembelea marafiki zao Sijali na Furaha. Furaha na Sijali wamewaandalia ratiba ya vitu vya kufanya siku nzima, inawalazimu Kinara na Maua kulala huko. Muda wa kulala umefika, Kinara anamuonyesha Sijali jinsi ya kufunga chandarua ili waweze kulala. Kinara anagundua kulala ndani ya chandarua kila siku sio umuhimu kama chandarua hicho hakitachomekwa vizuri chini ya tandiko.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1. Maua na Kinara walikuwa wanasafiri kwenda wapi?
   (***Jibu sahihi:*** Kijiji cha akina Furaha na Sijali)
2. Sijali na Kinara walilala kwenye kitanda gani?
   (***Jibu sahihi:*** Kitanda cha teremka tukaze)
3. Kwanini Sijali hakutundika chandarua chake?
   (***Jibu sahihi:*** Kwasababu aliona uvivu)
4. Ni hatua gani Kinara alifuata ilikutundika chandarua?
   (***Jibu sahihi:*** Kwanza unakikuchunjua chandarua na kukinyoosha kwenye kila pembe nne ya mahali unapolala kama hivi. Kisha tunafunga kamba kwenye kila pembe nne za chandarua.)
5. Kwanini mbu walikuwa wanapenya chini ya kitanda?
   (***Jibu sahihi:*** Kwasababu hawakuweka tandiko lolote juu ya kitanda)

### Zoezi la 11: Hatua za kutundika chandarua

Anza kwa kuwaonyesha watoto picha namba **6**.

**Sema:** Leo tutajadiliana kuhusu hatua za kutundika chandarua. Tutazitaja kwa mpangilio, kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho.

**Sema:** Ziko hatua nne.

1: Waonyeshe washiriki picha namba **6**, waulize je wameelewa picha inaonyesha nini?

2: Ili kuhakikisha wameelewa, Uliza, je picha hiyo inaonyesha nini?

(***Jibu sahihi:*** Inaonyesha familia inatundika chandarua kwa kusaidia)

Kama watakuwa wamejibu kwa usahihi endelea na maswali hapo chini, kama hawakujibu kwa usahihi toa maelezo ya hii picha.

1. **Uliza** huku unawaonyesha picha namba **6**
   - Kwakuangalia picha hii, unakumbuka ni hatua gani ya kwanza ya kutundika chandarua?
     (***Jibu sahihi:*** unakunjua chandarua, na kukitandaza juu ya usawa wa kona nne za sehemu ya kulala)
   - Hatua ya pili?
     (***Jibu sahihi:*** kufunga kamba pande nne za chandarua)
   - Hatua ya tatu?
     (***Jibu sahihi:*** kufunga kamba kwenye kona nne za chandarua na kuhakikisha chandarua kinafikia tandiko na kwa urahisi)
   - Hatua ya nne je?
     (***Jibu sahihi:*** unatundika/unafunga chandarua juu ya eneo la kulala pande zote nne )

2: **Uliza,** kuna anayetaka kuongeza hatua nyingine? Kama kuna mtoto ana hatua nyingine mpe nafasi aiseme na wenzake waijadili.



### Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Ni muhimu kutundika chandarua kwa usahihi ili iwe rahisi kukichomeka na kuzuia mbu wasiingie kwenye chandarua.



**Picha namba 6**

Sehemu ya 12:

# Siri ya **chandarua**

**Zawadi, Tumaini na Pipi wanakosa redio ya kusikiliza kipindi cha Patapata. Tumaini anawapeleka chumbani kwake kuwaonyesha jinsi alivyotundika chandarua chake. Tumaini anakumbushwa hatua ya muhimu ya kufanya ambayo ni kuhakikisha pande zote za chandarua zimechomekwa vizuri chini ya sehemu anayolala.Tumaini anamkumbusha Bonye kuchomeka chandarua chake, ila Bonye anasahau kuchomeka chandarua chake.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Tumaini aliwapeleka wenzake chumbani kwake wakaone nini?
(***Jibu sahihi:*** Wakaone jinsi alivyotundika chandarua alichogawiwa shuleni)
2) Nani alimsaidi Tumaini kutundika chandarua chake vizuri?
(***Jibu sahihi:*** Mama yake, baba yake na Bonye)
3) Ni hatua gani za kufuata ili kuchomeka chandarua kabla ya kulala?
(***Jibu sahihi:*** Unatakiwa kuchomeka sehemu zote nne za chandarua ziingie chini ya sehemu unayolala)
4) Bonye alisahau kufanya nini kabla ya kulala?
(***Jibu sahihi:*** Alisahau kuchomekea chandarua chake)

## Zoezi la 12: Igizo la uchomekeaji chandarua

**Leo tutaigiza maigizo mawili na kila igizo tutalijadili.**

### Igizo la 1

**Sema:** Igizo la kwanza linasema hivi, Mtoto amelala kwenye chandarua ambacho hakikuchomekewa vizuri na mbu amengia kwenye chandarua.

**Andaa watakao igiza**

1) **Sema:**
   - mtoto mmoja ajitolee kuigiza kama mtoto aliyelala kwenye chandarua ambacho hakikuchomekwa vizuri.
   - Watoto wengine watatu waigize kama mbu.
   - Waliobaki baadhi yao watakuwa chandarua.
2) Sasa yule ambaye ni mtoto alale chini.
3) **Sema:** Wale ambao ni chandarua washikane mikono kwa kumzunguka yule aliye lala chini.
4) **Sema:** Sasa mtoto mmoja kati ya wale ambao ni chandarua aachie mkono mmoja wa mwenzake.
5) **Sema:** Hapa ndipo itakapo kuwa sehemu ambayo haikuchomekewa vizuri kwenye tandiko
6) **Sema:** Watatu ambao ni mbu watakuwa wanawazunguka wale walioshikana mikono, kutafuta mahali pa kuingilia ndani ya mduara.
7) Mmoja wa wale mbu, ataona pale ambapo mmoja hakushika mkono na atapitia hapo kuingia katikati ya mduara na kumgusa mtoto aliyelala.
8) **Uliza** je, igizo hilo limewafundisha nini?

   (***Jibu sahihi:*** Kama chandarua haitachomekewa vizuri, kitaacha nafasi ya mbu kuingia ndani ya chandarua)

### Igizo 2:

Igizo la pili linasema hivi, mtoto amelala kwenye chandarua kilichochomekwa vizuri, mbu wanajaribu kuingia lakini wanakosa, wengine wanatua kwenye chandarua na kufa.

**Andaa watakao igiza:**

1) **Sema:**
   - Mtoto mmoja ajitolee kuigiza amelala
   - Watoto wengine watatu wajitolee kuigiza kama mbu
   - Watoto wengine waigize kuwa chandarua.

**Hakikisha kila mtoto anapata nafasi ya kushiriki moja ya maigizo haya mawili.**

2) **Sema:** Yule anayeigiza kama mtoto alale chini kama walivyofanya kwenye igizo la kwanza.
3) Wale ambao ni chandarua watashikana mikono kumzunguka yule mtoto aliyelala chini. Wote watakuwa wameshikana mikono.
4) Sasa wale watatu ambao ni mbu watakuwa wanazunguka ule mduara, wakitafuata mahali penye tundu ili waingie katikati ya mduara.
5) Mbu wengine waendelee kuzunguka watoto walioshikana mikono, kutafuta mahali pakuingilia bila mafanikio.

   Sasa waulize je, igizo hilo limewafundisha nini?
   (***Jibu sahihi:*** chandarua kikichomekwa vizuri mbu hawataingia kwenye chandarua)

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Kabla ya kulala, hakikisha umechomekea vizuri chandarua chako pande zote kwenye sehemu ya kulala, inaweza ikawa godoro, ngozi, kitanda cha kamba au mkeka. Ukichomeka vizuri unazuia mbu wasiweze kuingia kwenye ya chandarua na kukuuma.

Sehemu ya 13:

# Mzee **Limumi**

**Mwalimu mkuu anagundua vyandarua viwili vilivyobaki vimeibiwa katika mazingira ya ajabu sana. Pipi na wenzake wanafanya uchunguzi na kuja kujua mwizi wa vyandarua ni nani. Mwalimu mkuu anaita kikao cha dharaua na kumtaja mwizi. Bwana Limumi anajitetea na kueleza kwanini alifanya hivyo.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa:


Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kwanini Bi Kitonga na mwalimu mkuu walikuwa wanamuogopa Pipi?
(***Jibu sahihi:*** Kwa sababu alikuwa akiwakumbusha kulala kwenye chandarua kila siku)
2) Je shuleni kulitokea nini?
(***Jibu sahihi:*** Wizi wa chandarua)
3) Tumaini, Zawadi na Pipi walidhani nani aliimba vyandarua?
(***Jibu sahihi:*** Wachawi)
4) Nani aliiba chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Mlinzi wa shule, mzee Limumi)
5) Je ni kwanini aliiba vyandarua?
(***Jibu sahihi:*** Kwa sababu wao waligawana na yeye alinyimwa chandarua)

## Zoezi la 13: Kulala kwenye chandarua


**Waonyeshe watoto picha namba 7, halafu waulize maswali yaliyo nyuma ya picha.**

1) Unaona nini kwenye picha ya kwanza?
(***Jibu sahihi:*** Mtoto amelala bila kushusha chandarua, mbu anamuuma)
2) Kwa nini mtoto anaugua malaria mara kwa mara?
(***Jibu sahihi:*** Kwasababu hashushi chandarua kila siku, mbu wanamuuma.
3) Je, nini kitu gani ambacho mtoto hafahamu kuhusu malaria?
(***Jibu sahihi:*** Hafahamu kuwa hata mbu mmoja anatosha kuambukiza malaria)
4) Ili mtoto aepukane na kuugua malaria anapaswa kufanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Anatakiwa kushusha na kuchomeka chandarua chake kila siku)



## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Hakikisha unalala kwenye chandarua chenye dawa kila siku hata kama kuna mbu wachache, mbu mmoja anatosha kukuambukiza malaria. Kama huwezi kushusha na kuchomeka chandarua chako, mkumbushe mzazi, mlezi, kaka au dada akusaidie kushusha chandarua kabla hujalala.



**Picha namba 7**

Sehemu ya 14:

# Kinara na Bonye

**Kinara na Bonye wako hospitali, Zawadi , Pipi, Tumaini na Maua wameenda kuwaona. Kinara anawaeleza wenzake kujikinga na malaria sio tu kulala ndani ya chandarua bali pia ni muhimu kuchomeka vizuri chandaru ili kuzuia mbu wasipenye. Bonye anawaeleza wenzake ni nini atakachokifanya ili asimumwe tena malaria. Mzee mmoja anawashangaa hao watoto na anawauliza ni wapi wamejifunza kuhusu umuhimu wa kulala ndani ya chandarua kila siku na kukichomeka chandarua vizuri.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kinara na Bonye walikuwa wanaumwa nini?
(*Jibu sahihi:* malaria)
2) Baada ya safari, Kinara alijifunza nini kutoka kwa akina Sijali?
(*Jibu sahihi:* Kwamba hata ukitundika chandarua kama hukukichomeka vizuri kwenye tandiko la kulalia ni kazi bure.)
3) Bonye aliahidi kufanya nini ili asiumwe tena malaria?
(*Jibu sahihi:* Atahakikisha mara mbili-mbili kwamba amechomeka vizuri chandarua )
4) Kwanini ni muhimu kuchomeka chandarua vizuri hata kama umelala ndani ya chandarua?
(*Jibu sahihi:* Kwasababu ukichomeka chandarua vizuri, utazuia mbu kuingia kwenye chandarua)
5) Ni wapi Zawadi na wenzake wamejifunza kuhusu umuhimu wa kuchomeka chandarua vizuri?
(*Jibu sahihi:* Huwa wanakutana pamoja na kusikiliza kipindi cha redio cha Patapata)

## Zoezi la 14: Igizo la mfano wa chandarua

**Leo tutafanya igizo la mfano wa chandarua.**

**Igizo linasema hivi:**
Watoto wawili kila moja kwenye kitanda chake, wamelala kwenye chandarua, mbu wanarukua ruka toka kwa mtoto mmoja kwenda kwa mwingine lakini wanashindwa kuwang'ata kwa kuwa kila mtoto yuko kwenye chandarua.

**Andaa watakao igiza:**

1) **Sema:** Watoto wawili wajitolee igiza wamelala ndani ya chandarua, wengine watatu wajitolee kuigiza kama mbu, wengine waigize kuwa chandarua.
2) Hakikisha kuna watoto wakutosha kuwazunguka kama chandarua.
3) **Sema**: Wale watoto wawili wanaoigiza kama watoto wanaolala kwenye chandarua walale chini sehemu mbali mbali kidogo ili kila mmoja aweze kuzungukwa na wenzake.
4) Wale ambao ni chandarua watashikana mikono kumzunguka kila mtoto aliyelala chini. Kwahiyo kutakua na duara mbili
5) Sasa wale wawili ambao ni mbu watakuwa wanazunguka ile miduara miwili, wakitafuata jinsi ya kuwafikia wale waliolala katikati.
6) **Uliza:** Kwanini wale mbu wameshindwa kuwafikia wale walio katikati.
(*Jibu sahihi:* kwa sababu wamezungukwa na wale walioshikana mikono).
7) **Sema:** Hivyo ndivyo ilivyo vigumu kwa mbu kuweza kumuuma mtu aliyelala kwenye chandarua.
8) **Sema:** Kama walivyolala kwenye miduara miwili, inaonyesha kuwa kila mtu akilala kwenye chandarua, mbu atakosa mtu wakumuuma na kumuambukiza ugonjwa wa malaria. Hii itazuia kabisa maambukizi ya malaria katika jamii.
9) **Uliza:** umejifunza nini kwenye hili igizo?
(*Jibu sahihi:* Ni umuhimu kila mtu kwenye jamii kulala kwenye chandarua kila siku) .

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Watoto pia mnaweza kuwahamasisha watoto wenzenu kuhusu umuhimu wa kila mtu kulala kwenye chandarua ili jamii ijikinge na ugonjwa wa malaria. Wanafunzi mnaweza kushiriki kupambana na malaria kwa kujiunga kwenye klabu za malaria au kuanzisha klabu za malaria kama hazipo shuleni. Kabla ya kuanzisha klabu shuleni onana na mwalimu wako wa afya ili akupe maelekezo

Kwenye klabu mtawafundisha wenzenu na mtajadiliana kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua. Mnaweza pia kuunda vikundi vidogo vidogo nyumbani na kusiliza kipindi cha patapata kila Jumamosi.

Sehemu ya 15:

# Chandarua cha familia ya Bonye

**Mwalimu Chewa anamkabidhi Bonye chandarua na kumsisitizia kwamba chandarua hicho sio chake peke yake bali ni cha familia nzima na ahakikishe kimetumika. Maua na Kinara wapo stesheni wanarudi shule. Bi Kiduku anashidwa kumpa Maua namba yake ya simu kwani haijui ye mwenyewe. Zawadi anatumia simu ya Bi Kiduku nakumpigia Bibi Kinara iliapate namba ya Bi Kiduku.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kwanini Bonye hakupata chandarua wakati wenzake walipogawiwa?
(***Jibu sahihi:*** Jina lake halikuwepo kwenye orodha)
2) Bonye alisema akifika nyumbani atafanyaje?
(***Jibu sahihi:*** Atahifadhi chandarua vizuri chumbani kwake)
3) Mwalimu Chewa alimfahamisha nini Bonye kuhusu chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Akifika nyumbani amkabidhi mzazi au mlezi wake kwa kuwa chandarua ni cha familia nzima)
4) Maua alikuwa anaondoka kwenda wapi?
(***Jibu sahihi:*** Alikuwa anarudi shule)
5) Maua alimuasa nini Zawadi ?
(***Jibu sahihi:*** Wasiache kikundi chao. Waendelee kukutana kila jumamosi kusikiliza kipindi cha redio cha Patapata na pia kuelimishana kuhusu mambo mbalimbali ya ugonjwa wa malaria)

## Zoezi la 15: Igizo la mfano wa chandarua

Leo tutafanya igizo la chandarua cha Bonye. Igizo linasema hivi, Zawadi na Bonye wamegawiwa vyandarua shuleni, Bonye anadhani kile chandarua ni cha kwake binafsi, Zawadi anamkumbusha kuwa chandarua kile ni kwa ajili ya familia. Bonye anapokifikisha chandarua nyumbani, baba yake anaamua kumpa shangazi yake Bonye kwa sababu familia ya bonye wanavyo vya kutosha na shangazi yake hana chandarua kabisa.

### Andaa waigizaji

1) **Sema:** Watoto wawili wajitolee kuigiza, mmoja awe Zawadi na mmoja awe Bonye (hivyo mmoja awe wa kike na mmoja wa kiume). Mtoto mwengine ajitolee kuigiza kama mzazi na wengine wanne waigize kama rafiki zake Bonye
2) **Sema:** Mtaigiza kama ilivyoandikwa hapo chini. (Wape muda wahusika kupitia sehemu zao)
3) **Sema:** Sio lazima kukariri maneno kama yalivyoandikwa ila kinachotakiwa ni maana ya igizo ibaki pale pale.

**Zawadi:** Bonye unakumbuka tuliambiwa ukipokea chandarua unakipeleka wapi?

**Bonye:** Ukipokea chandarua unaendanacho nyumbani

**Zawadi:** Halafu?

**Bonye:** Halafu nini? Si nakitumia mimi?

**Zawadi:** Hapana. Chandarua ni cha familia

**Bonye:** Nampa nani sasa?

**Zawadi:** Ukifika nyumbani umkabidhi mzazi au mlezi.

**Bonye:** Sawa nitafanya hivyo.

(Bonye amefika nyumbani)

**Bonye:** Shikamoo baba. Leo tumegawiwa vyandarua shuleni

**Mzazi:** Marahaba. Afadhali tumepata chandarua nyingine, kwa maana shangazi yako hana chandarua.

**Bonye:** Sawa baba, hata shuleni tuliambiwa, kama nyumbani vyandarua vinatosha na tuna cha ziada tumpe ndugu au ajirani ambae hana chandarua

(Bonye na wenzake wanacheza)

**Rafiki wa Bonye:** Bonye, chandarua chako nani anakitumia?

**Bonye:** Nimekipeleka kwa shangazi, alikua hana chandarua.

**Rafiki wa Bonye:** Mi cha kwangu anatumia mdogo wangu.

**Mwisho wa igizo**

**Sasa ongoza majadiliano kwa maswali yafuatayo.**

1. Kwanini Bonye alimkabidhi baba yake chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Kwasababu chandarua ni kwa ajili ya familia)
2. Kwanini baba alisema chandarua kile apewe shangazi yake Bonye?
(***Jibu sahihi:*** Kilikuwa chandarua cha ziada na shangazi alikuwa hana chandarua)

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Ukifika nyumbani mueleze mzazi/mlezi na rafiki yako ulichojifunza leo. Vyandarua mtakavyogawiwa shule ni kwa ajili ya familia zenu na jamii nzima. Mwanafunzi utakipokea na kukipeleka nyumbani. Mtu yoyote kwenye familia asiye na chandarua anaweza kukitumia.

Sehemu ya 16:

# Kishada cha Pipi

**Pipi na Tumaini wako kilimani wanachezea kishada. Tembe anatungua kishada cha Pipi na kinaangukia kwenye shamba cha Mzee Chanjagaa. Zawadi anajitolea kwenda kukifuata kishada kwani wengine wote wanamuongopa Mzee Chanjagaa. Zawadi anapata wazo lakumpelekea Mzee Chanjagaa chandarua ili apatiwe kishada cha Pipi.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kishada cha Pipi kiliangukia wapi?
(***Jibu sahihi:*** Kwenye shamba la mzee Chanjaga)
2) Kwanini watoto waliogopa kwenda kukichukua kishada cha Pipi?
(***Jibu sahihi:*** Mzee Chanjagaa alishawahi kupiga mjusi kwa gobole/ anakaa peke yake mabondeni)
3) Zawadi alitoa wazo gani ilikumsaidia Pipi kupata kishada chake?
(***Jibu sahihi:*** Kumuomba Bi Kiduku ruhusa ya kumpa mzee Chanjagaa chandarua chao cha ziada)
4) Kwanini Mzee Chanjagaa alichukua chandarua Zawadi alichomletea?
(***Jibu sahihi:*** Kwasabau chandarua chake kilikuwa kimechakaa na cha muda mrefu)
5) Zawadi aliwaambia nini wenzake alivyotoka kwa mzee Chanjagaa?
(***Jibu sahihi:*** Mzee Chanjagaa amealika wote kurudi siku nyingine)

## Zoezi la 16: Mchezo wa kuvuta kamba

**Andaa kamba kwa ajili ya huu mchezo.**

**Andaa watakao igiza:**

1) Leo tutacheza mchezo wakuvuta kamba.
2) **Sema:** Jigaweni katika makundi mawili, kila kundi lichague jina lake.
Chora mstari katikati ya makundi haya mawili, wape kamba
3) **Sema:** Kila timu ishike mwisho wa hii kamba, nitahesabu 1hadi 3 mtaanza kushindana kuvuta kamba, kila kundi upande wake. Muwe makini msivuke mstari. Kundi litakalo vuka mstari litakua limeshindwa
4) **Sema:** 1, 2, 3 vuta.
5) Watoto wavutane hadi wapatikane watakao vuka mstari. Waambie wale waliovuka mstari wameshindwa na malaria lakini wako katika jamii moja.
6) **Sema:** Sasa makundi yote mawili muungane, mkae katika mduara na muanze kuvuta kamba kwa pamoja mkielekea upande mmoja.
7) Hesabu 1, 2, 3 vuta.
8) **Sema:** Pamoja timu zote ni washindi, hivyo wote kwa pamoja mmeishinda malaria. Hii ni jamii nzima.

**Hatua 1: Waambie sasa tunaanza kujadili mchezo wa kwanza;**

1) **Uliza;** umejifunza nini katika mchezo wa kwanza?
(***Jibu sahihi:*** Kuna timu iliyoshinda na iliyoshindwa)
2) **Sema:** Timu zile mbili ni watu walio katika jamii moja na wanapigana vita na ugonjwa wa malaria wengine wanalala kwenye vyandarua na wengine hawalali kwenye chandarua.
3) Kwa maelezo haya mmejifunza nini?
(***Jibu sahihi:*** Waliovutwa ni wale wasiolala kwenye chandarua na wamepata malaria)
4) **Uliza:** Kuna tatizo gani kama kuna watu wenye vimelea vya malaria kwenye jamii?
(***Jibu sahihi:*** Wataawaambukiza wale wasio na vimelea vya ugonjwa wa malaria)

**Hatua 2: Sema sasa tunajadili mchezo wa pili:**

1) Wakumubushe kwa kuuliza, Nani anakumbuka kwenye mchezo wa pili nini kilitokea?
(***Jibu sahihi:*** Walivuta kamba katika mduara kwa kwenda upande mmoja)
2) **Uliza:** Umejifunza nini kwenye mchezo wa pili?
(***Jibu sahihi:*** kushirikiana kwa pamoja kunaleta mafanikio na kutapunguza maabukizi ya malaria)
3) **Sema:** Kuvuta kamba kwa pamoja katika mduara ni kushirikishana kwa kupeana vyandarua.
4) **Sema:** Tushirikiane kupambana na ugonjwa wa malaria kwa kuhakikisha kila mtu kwenye jamii analala kwenye chandarua. Kama unachandarua cha ziada mpatie jirani yako asiyekua nacho.
5) **Sema:** Mbu anayeeneza ugonjwa wa malaria hana mipaka.

***Washukuru kwa kushiriki katika michezo hiyo.***

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Mwanafunzi shiriki kutokomeza malaria kwa kuwatambua majirani, rafiki na ndugu ambao hawana vyandarua. Mtaarifu mzazi au mlezi, kama nyumbani kuna vyandarua vya ziada mumpatie jirani asiyekuwa nacho.

Sehemu ya 17:

# Hadithi za Mzee Chanjagaa

**Mzee Chanjagaa anawakaribisha Zawadi, Tembe na Pipi nyumbani kwake kwani wamekuja kumtembela. Mzee Chanjagaa anawasimulia hadithi ya vihoja vya sungura na paka kufukuzwa porini na wanyama wenzake.Watoto wanafurahi kusikiliza hadithi hiyo nzuri ambao wanajifunza umuhimu wa kushirikiana na wenzao hasa kwenye jamii katika kupambana na tatizo lolote linaowathiri kama malaria.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Zawadi alikuwa anawaambia wenzake waende wapi?
(***Jibu sahihi:*** Kwa mzee Chanjagaa)
2) Mzee Chanjagaa aliwasilimulia hadithi kuhusu nini?
(***Jibu sahihi:*** Sungura ambaye hakutaka kusaidiana na wanyama wenzake katika kuchimba bwawa kubwa ili wapate maji)
3) Watoto walijifunza nini la muhimu kutokana na hiyo hadithi?
(***Jibu sahihi:*** Umuhimu wa kuwa na umoja/ kusaidiana na kushirikiana)
4) Zawadi alisema nini kuhusu umuhimu wa kushirikiana?
(***Jibu sahihi:*** Ni muhimu kushirikiana na kumgawia ndugu, rafiki au jirani asiyekuwa na chandarua kwani kama kila mtu akiwa analala ndani ya chandarua hapa kijijini mbu hataweza kueneza ugonjwa wa malaria)

## Zoezi la 17: Mchezo wa miduara

### Leo mtacheza mchezo wa kuchangamsha mwili na akili.

1) **Sema:** Simameni na kila mmoja ulipo simama uchore mduara kuzunguka miguu yako. Mduara wako ni chandarua chako.
2) **Sema:** Wote tokeni nje ya mduara, msimame mbali kidogo ya miduara yenu.
3) **Sema:** Utafuta mduara wa mmoja wao. Kwa hiyo mmoja hana tena mduara
4) **Sema:** Nitakapo piga kofi, kimbieni mrudi kusimama ndani ya mduara wako uliochora. Atakaye kosa au kuchelewa kuingia kwenye mduara atakaa pembeni.

   Endelea na zoezi la kufuta mduara moja na kuwaambia kila mmoja arudi kwenye mduara wake. Lengo ni kila mara awepo ambaye hatakuwa na mduara wa kuingia
5) Endelea na zoezi hilo mpaka wapatikane washindi, angalau wabaki 4 au 5, hao watangaze kuwa ni washindi. Wapongeze kwa kuwa washindi.
6) **Sema:** Miduara mliochora ni vyandarua , wale wanaokosa mduara na kutoka nje ya mchezo ni wale waliokuwa na vyandarua lakini sasa hawana tena kwa sababu mbalimbali mfano kuchakaa, kuchanika, kuongezeka idadi ya watu katika familia n.k. wale walio na vyandarua wanaendelea kuwa katika mduara mpaka mwisho
7) **Sema:** Ili kujikinga na malaria lazima kila mtu alale kwenye chandarua kila siku, hivyo wale wote wasio na vyandarua wanahatari ya kuwaambukiza wengine malaria.
8) **Sema:** Wale waliotoka kwenye mchezo, hawa wako katika hatari ya kupata malaria.
9) **Sema:** Ili kutokomeza malaria ni lazima wote tuwe washindi.
Uliza, tufanye nini ili watu wote wabaki katika mduara? Maana kubaki katika mduara ndio ushindi.
(***Jibu sahihi:*** Kutambua wale wasiokua na chandarua na pili ni kuwapa vyandarua)
10) **Sema:** Katika mchezo huu tumepata washindi lakini malaria haina mshindi mmoja ua wawili, ni lazima jamii nzima wawe washindi, kwahiyo kama familia ina vyandarua vya kutosha, kile cha ziada mpatie jirani yako asiyenacho.

***Washukuru wa kushiriki zoezi hili.***

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Watakaporudi nyumbani wafahamishe wazazi/walezi kama kuna chandarua cha ziada wampatie jirani asiyenacho. Kwa njia hii jamii nzima itakua imejikinga na ugonjwa wa malaria

Sehemu ya 18:

# Ajali ya Bi Kiduku

**Zawadi, Pipi na Tumaini wako mabondeni wanamfundisha Bi Kiduku kuendesha baiskeli. Huko wanakutana na Mzee Chanjagaa ambae anamshamgaa Bi Kiduku kuwa na umri wake bado ajui kuendesha baiskeli. Bi Kiduku anaamua aendeshe baiskeli peke yake, ila anaanguka nayo na kuchumbua goti lake. Zawadi na wenzanke wanampeleka hospitali ili atibiwe.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Bi Kiduku alikuwa anajifunza kufanya nini?
(*Jibu sahihi:* Kuendesha baiskeli)
2) Kwanini Bi Kiduku alipelekwa hospitali?
(*Jibu sahihi:* Alichubuka goti na damu ikatoka/ aliumia)
3) Kwanini mwalimu Sango alishikwa na malaria?
(*Jibu sahihi:* Hakujua kwamba chandarua chake kilichanika)
4) Kwanini chandarua cha mwalimu Sango kilichanika?
(*Jibu sahihi:* Aliweka vitabu vyake na nguo juu ya chandarua)

## Zoezi la 18: Igizo la jinsi ya kutunza chandarua

**Leo tutafanya igizo la namna yakutunza chandarua.**

1) **Sema:** Watoto watatu mjitolee kuigiza.
2) Kaa pembeni na hao watoto watatu peke yao. Wasomee igizo la kila mmoja. Hakikisha wale wengine wote hawafahamu kitakachoigizwa.
3) Waambie watoto watatu kila mmoja aigize kwa vitendo igizo bila kusema moja kati ya hayo hapo chini.
4) Wape muda wa kuandaa maigizo yao

**Igizo 1:** Mtoto anachomeka chandarua ovyo ovyo bila uangalifu na chandarua kinachanika, anakagua chandarua chake, anasikitika kwa kuwa chandarua chake kina matundu.

**Igizo 2:** Mtoto anatundika chandarua, halafu anaweka vitabu na nguo juu yake, anaangalia chandarua chake nakuona kimechanika, anahuzunika.

**Igizo3:** Mtoto anachomekea chandarua chake kwa uangalifu, anakikagua chandarua chake,anagundua ni kichafu, anakifua na kuianika kivulini. Kimekauka na anakianua, anafurahi chandarua chake kipo katika hali nzuri.

5) Waambie washiriki wengine waangalie kwa makini jinsi wenzao anavyoigiza, kwa kuwa watatakiwa kueleza walikuwa wanaigiza nini.
6) Waambie wale watatu kila mmoja akimaliza kuonyesha igizo lake, awaulize washiriki wenzake wamejifunza nini katika igizo waliloona? Kama watakosea awape jibu sahihi.
   - **Mtoto wa 1:** Aulize, mmejifunza nini katika igizo hili?
     (*Jibu sahihi:* Kuchomekea chandarua ovyo ovyo bila ungalifu kunafanya chandarua kiwe na matundu au kichanike)
   - **Mtoto wa 2:** Aulize, mmejifunza nini katika igizo hili?
     (*Jibu sahihi:* Kuweka vitu kama vitabu na nguo juu ya chandarua kilichochomekwe vinaweza kuchana chandarua)
   - **Mtoto wa 3:** Aulize, mmejifunza nini katika igizo hili?
     (*Jibu sahihi:* Ukichomeka chandarua kwa uanagalifu, ukakifua kinapochafuka na kuanika kivulini kinadumu muda mrefu. Hakiwezi kuchanika)

### Hitimisha kwa kuwaeleza :

**Jinsi ya kutunza chandarua:**

1) Hakikisha unakunja kwa uangalifu chandarua yako unapo amka.
2) Kabla ya kulala, hakikisha unachomekea kwa uangalifu chandarua chako kwenye godoro, mkeka, ngozi au sehemu yoyote yakulalia.
3) Usiweke vitu kama vitabu, nguo, au vitu vyenye ncha kali juu ya chandarua kilichotundikwa, vinaweza kuchana chandarua chako.
4) Fua chandarua chako kinapochafuka na kianike kwenye kivuli.

**Sema:** kama ukitunza chandarua chako utajikinga na malaria na utaikinga jamii nzima malaria.

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Kama mlivyojifunza kwenye igizo, mkirudi nyumbani mzungumze na wazazi na marafiki zenu jinsi ya kutunza chandarua. Ni muhimu kutunza chandarua ili kuikinga familia na mbu waenezao ugonjwa wa malaria.

Wale wote ambao nyumbani kuna vyandarua vilivyo na matundu, waje kila mmoja na chandarua kimoja, kwenye kipindi cha wiki ijayo mtajifunza kwa vitendo jinsi ya kushona chandarua chenye matobo. Vile vile mje na uzi na sindano.

**Ujumbe kwa CCA:** Andaa chandarua kimoja kisafi lakini kilichotoboka kwaajili ya kuwaonyesha mfano watoto namna yakushona chandarua

Sehemu ya 19:

# **Zawadi** Mwanasoka

**Bi Kiduku anamuonya Zawadi kuhusu kucheza mpira wa miguu na wavulana kwani watamuumiza. Bila anakasirika na kuchukua mpira wake baada ya timu yake kufungwa. Zawadi anamshawishi Doto waende wakasikilize kipindi cha Patapata kwenye kikundi chao. Kwenye kipindi wanajifunza jinsi ya kufanya iwapo wakikuta chandarau chao kimechanika au kutoboka**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kwanini Bi Kiduku alikuwa hataki Zawadi acheze mchezo wa mpira?
(***Jibu sahihi:*** Wavulana watakuja kumuumiza)
2) Baada ya mchezo Zawadi alimwambia Doto wanaenda wapi?
(***Jibu sahihi:*** Wanaenda kufanya mkutano wa kikundi chao)
3) Kwenye kikundi hicho walikuwa wanafanya nini?
(***Jibu sahihi:*** Wanakutana kila Jumamosi kusikiliza kipindi cha Patapata kwenye redio, halafu baadae huwa wanaongea na wazazi wao kuhusu mambo waliyosikia na kujifunza kwenye kipindi cha siku hiyo.)
4) Mtangazaji alisema ni kuhusu iwapo chandarua kikitunza vizuri?
(***Jibu sahihi:*** Utakaanacho kwa muda mrefu sana na kujikinga wewe pamoja na jamii nzima dhidi ya ugonjwa wa malaria)

## Zoezi la 19: Kushona chandarua

**Kabla ya zoezi anza kwa kuuliza kama wamekuja na vyandarua, uzi na sindano kama ulivyoagiza wiki iliyopita.**

1) Kama wameleta vyandarua, zoezi hili utaliongoza kwa pamoja wakati kila mmoja mwenye chandarua akifuatisha kile unachosema na kufanya kwa vitendo. Wale wasiokua na chandarua wataangalia wenzao wanavyofanya
2) Sema: Anza kwa kukagua chandarua ili kubaini matundu, hivyo kila mmoja mwenye chandarua akiangalie chandarua yake na kubaini matundu yako sehemu gani.
3) Uliza: Kawaida ukiona tundu kwenye chandarua huwa unafanya nini? ( Sikiliza majibu yao mfano, kushona, kufunga fundo, kufunga kwa uzi na kuacha hivyo hivyo).
4) Sema: Leo mtajifunza jinsi ya kushona chandarua kilichotoboka, tutashona pale palipochanika au penye tundu, tusifunge fundo, usikifunge kwa uzi au kuacha matundu yaendelee kuwa makubwa.
5) Sema: Sehemu yenye tundu au iliyochanika itashonwa kwa kutumia uzi na sindano, sasa onyesha kwa vitendo. Shona sehemu moja yenye tundu kwenye chandarua chako ili watoto waone mfano
6) Kama ni wengi wamekuja na vyandarua wape muda na wao kushona moja ya tundu lililopo kwenye vyandarua vyao.
7) Sema matundu yaliyobaki watakwenda kumalizia nyumbani, lakini kama muda unatosha wanaweza kufanya zoezi hili na kulikamilisha hapo hapo, angalia hizo chandarua zao kama zina matundu mengi.
8) Kwa uangalifu kagua vyandarua walivyoshona, kwasababu vyandarua nyingine zinaweza kuwa na matundu mengi sana na zimechoka, kiasi kwamba sio rahisi kushona.
9) Hii itawasaidia nao kubaini ni chandarua gani kinaweza kushona na kipi kimechoka kinahitaji kubadilishwa.
10) Uliza kama kila mmoja ameelewa jinsi ya kushona chandarua kilichotoboka, hasa wale ambao hawakuja na chandarua fuatilia kama wameelewa.

**Mwisho hitimisha kwa kusema:**

- Shona chandarua chako haraka iwezekanovyo mara baada ya kugundua kimetoboka
- Ili kuzuia chandarua chako kuchanika mara kwa mara hakikisha unachomekea chandarua kwa uangalifu wakati kabla ya kulala.
- Usiweke vitu juu ya chandarua kilicho tundikwa kwa sababu vinaweza kuchana chandarua chako. Vitu kama vitabu, nguo na vitu vyenye ncha kali
- Unauhakika wa kukaa na chandarua chako kwa muda mrefu kama utakua wanakishona mara tu kinapo chanika.
- Sisistiza kuwa chandura ni kitu cha thamani hivyo kinatakiwa kutunzwa.

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Mkirudi nyumbani kila mmoja awashirikishe wazazi/walezi na marafiki kile alichojifunza kuhusu jinsi ya kushona chandarua. Anaweza kukagua vyandarua vyote ndani ya nyumba ili kubaini vyenye matundu na kuvishona mwenyewe au omba msaada kwa mzazi ili akusaidie kushona.

## Kumbuka:

Ili chandarua kidumu kwa muda mrefu, unahitaji kuwa muangalifu wakati wa kuchomekea, na ni muhimu kukikagua, na kukishona haraka pale unapogundua kimechanika.

Sehemu ya 20:

# **Vipele** vya **Bi Kiduku**

**Zawadi anagundua kuwa chandarua cha Bi Kiduku kimetoboka na anataka akishone ila Bi Kiduku anakataa kumsikiliza. Kesho yake asubuhi Bi Kiduku anaamka na vipele usoni, anashangaa vimetokea wapi wakati alilala kwenye chandarua. Zawadi anamwambia kuwa mbu walipita kwenye kitobo ambacho alikataa kishonwe, na anaendelea kumuelewesha ni jinsi ngani anaweza kuziba hicho kitobo.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Chandarua cha Bi Kiduku kilikuwa na tatizo gani?
(***Jibu sahihi:*** Kimetoboka)
2) Zawadi alimwambia Bi Kiduku afanyaje nini kuhusu chandarua chake?
(***Jibu sahihi:*** Akishone mara moja)
3) Kwanini Bi kiduku aliamka na vipele usoni kwake?
(***Jibu sahihi:*** Mbu waliamuuma)
4) Mbu waliomuuma Bi Kiduku walipitia wapi?
(***Jibu sahihi:*** Kwenye shimo lililokuwepo kwenye chandarua chake)
5) Kushona chandarua unatakiwa ufanyaje?
(***Jibu sahihi:*** Kushona kwa uzi na sindano)

## Zoezi la 20: Utunzaji wa chandarua

**Waonyeshe watoto picha namba 8. Halafu uliza maswali yafuatayo**

1) Unaona nini kwenye picha A?
(***Jibu sahihi:*** Wameamka wanakunja chandarua).
2) Unaona nini kwenye picha B?
(***Jibu sahihi:*** Anachomeka kundarua kwa uangalifu ili kisichanike)
3) Unaona nini kwenye picha C?
(***Jibu sahihi:*** Anafua chandarua na anakianika kivulini)
4) Baada ya zoezi hili la kutambua picha, waulize ni wangapi wanadhani leo wamejifunza kitu kipya? Dodosa ni nini ambacho amejifunza leo ambacho ni kipya kwake.





## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Leo mlikuwa mnajifunza namna ya kutunza chandarua. Mkirudi nyumbani, angalia kama chandarua chako ni kichafu kinahitaji kufuliwa. Zungumza na wazazi /walezi wako kuhusu namna ya kutunza chandarua na wasaidie kutunza vyandarua vyao. Waambie wazazi au mlezi kuwa ni muhimu kutunza vyandarua kwa sababu vitadumu kwa muda mrefu na vitawakinga na malaria, wao na jamii nzima.

**Picha namba 8**






Sehemu ya 21:

# Kazi ya **Kujitolea**

**Mwalimu Mkuu anawapa zoezi wanafunzi waende wakafanye kazi za kujitolea na kisha wajewaseme ni nini walichokifanya darasani. Wanafunzi wengi walionekana na kuwa na moyo wa kujitolea sana kasoro Bila ambae alikamatwa na kuchapwa sokoni kwani aliiba maembe ya watu. Mwalimu anawaambia ni muhimu kuwa na moyo wa kujitolea kwani utajenga uaminifu na kujifunza maarifa mengi.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Kwa nini mwalimu Sango hakuweza kufundisha kipindi chake cha historia?
(***Jibu sahihi:*** Alikuwa anaumwa malaria na kulazwa hospitali)
2) Mwalimu mkuu alisema nini kuhusu chandarua chenye dawa?
(***Jibu sahihi:*** Kinazua mbu na kujikinga na malaria na dawa haina madhara yoyote)
3) Kwa nini Zawadi hakuweza kwenda kujitolea kushona vyandarua vya majirani zake?
(***Jibu sahihi:*** Bi Kiduku alikwenda hospitali kuangalia hali yake, hivyo Zawadi alifanya kazi zote za nyumbani)
4) Baada ya kumaliza kazi zake, Zawadi alifanya kazi gani ya kujitolea?
(***Jibu sahihi:*** Alimpakiza mama mmoja kwenye baisikeli yake na kumpeleka hadi kwenye kituo cha afya.)
5) Mwalimu mkuu aliwaambia nini mwisho wa igizo?
(***Jibu sahihi:*** Katika dunia hii ni muhimu sana kusaidiana kwani kila mtu atahitaji msaada wa aina moja au nyingine katika maisha yake.)

## Zoezi la 21: Kweli, sikweli

**Sema:** Zoezi la leo ni la kupima uelewa kuhusu malaria. Nitasoma sentensi na nyie mtanijibu kwa kusema ni kweli au sio kweli.

1) **Sema:** Kwa kila swali wale mtakao jibu ni kweli watasimama upande wangu wa kulia na mtakao sema si kweli mtasimama upande wangu wa kushoto.
2) **Sema:** Tutajadili majibu yenu, waliojibu ni kweli mtasema kwasababu gani, vile vile mliosema si kweli mtasema kwasababu gani.

**Sasa soma sentensi ya kwanza**

4) Toa muda kwa washiriki kuchagua jibu na kuelekea upande wa jibu lao
5) Ongoza majadiliano kwa kuuliza mshiriki mmoja toka kila upande kwa nini amechagua jibu hilo.
6) Toa jibu sahihi kwa sentensi hiyo
7) Endelea na sentensi inayofuata na utaratibu ni ule ule mpaka umalize sentensi zote.

**Sentensi**

1. Vyandarua vyote vilivyo/ vitakavyo gawiwa shuleni vina dawa ya kudumu muda mrefu.
(***Jibu sahihi:*** Ni kweli)
2. Hata vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu vinatakiwa kuwekewa dawa mara baada ya kuvipata au kufua.
(***Jibu sahihi:*** Si kweli- dawa ile ni ya muda mrefu, hata baada ya kufua bado ina nguvu)
3. Ukifua chandarua chako unapaswa kukianika kivulini ili kulinda dawa isiishe nguvu.
(***Jibu sahihi:*** Ni kweli - jua linamaliza nguvu ya dawa)
4. Hakuna tofauti ya uwezo wakukukinga na malaria kati ya chandarua chenye dawa na kisicho na dawa
(***Jibu sahihi:*** Si kweli - chandarua chenye dawa kina kinga zaidi ya kile kisicho na dawa kwasababu dawa iliyo kwenye chandarua inaua mbu waenezao malaria).
5. Dawa iliyowekwa kwenye chandarua haina madhara kwa binadamu.
(***Jibu sahihi:*** Ni kweli - dawa hiyo ni maalum kwa ajili ya kuulia mbu aina anofelesi na imedhibitishwa na Wizara ya afya kuwa ni salama kwa afya ya watu wote hata watoto).
6. Kulala kwenye chandarua usiku sio kinga ya malaria kwa sababu unaweza kuumwa na mbu wakati wa mchana au jioni.
(***Jibu sahihi:*** Si kweli - kwa sababu mbu aina ya anofelesi aenezae vimelea vya ugonjwa wa malaria uuma wakati wa usiku ukiwa umepumzika.)

**Wapongeza kwa kushiriki zoezi hili.**

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Wakifika nyumbani, Wajulishe wazazi na marafiki kuwa vyandarua vinavyotolewa shule vina dawa ya muda mrefu, huitaji kuweka dawa tena. Ni muhimu kulala kwenye chandarua chenye dawa ili kujikinga na mbu waenezao malaria.

Sehemu ya 22:
# Bibi **Kizee**

**Bi Kiduku na Zawadi wako kwenye soko la samaki. Bi Kiduku anakataa kununua samaki kutoka kwa muuzaji kwasababu alitumia chandarua kwa kuvulia samaki. Zawadi anakubaliana na Tumaini kuwa baadae wataenda kwa Mzee Chanjagaa. Mzee Chanjagaa anafurahi sana kuwaona akina Zawadi pamoja na rafiki yao mpya Dotto, anawakaribisha na kuanza kuwasimulia hadithi zake.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Bi Kiduku alitumiwa nini?
(***Jibu sahihi:*** Hela kwenye simu)
2) Kwa nini Bi Kiduku alikataa kununua samaki kwa muuzaji?
(***Jibu sahihi:*** Kwa kuwa alitumia chandarua kuvulia samaki)
3) Tumaini na Zawadi walikubaliana baadae watakwenda kwa nani?
(***Jibu sahihi:*** Kwa Mzee chanjagaa)
4) Katika hadithi yule mke alichagua nini?
(***Jibu sahihi:*** Mumewe awe na kichwa kama cha kuku)
5) Ni kitu gani cha maana alichochagua Pipi?
(***Jibu sahihi:*** Kulala ndani ya chandarua kila siku asiumwe na mbu na kupata malaria)

## Zoezi la 22: Nyama, nyama

### Leo mtutacheza mchezo wa nyama! Nyama! Nyama!.

**Toa maelekezo ya jinsi mchezo unavyochezwa.**

1) **Sema:** Mchezo huu unachezwa kwa kuruka juu wakati wakumuitikia kiongozi. Kiongozi akisema nyama nyama, nyama wengine wanaitikia nyama! na kuruka juu. Unaruka kukubali kama nyama aliyotaja kiongozi inaliwa na watu. Kama sio kawaida nyama ile kuliwa na watu, basi hauruki wala hausemi nyama! Unakaa kimya. Atakaye ruka au kusema nyama wakati nyama iliyotajwa hailiwi na watu , anakua amekosea hivyo anatolewa kwenye mchezo.
2) **Sema:** Mkae kwenye mduara ili mchezo uanze.
3) **Sema:** Masharti ya huu mchezo kila nayekosea, anatolewa kwenye mduara atakaa katikati ya mduara ili kumsaidia kiongozi kuwabaini wanaokosea. Lengo ni kumtafuta mshindi.
4) Mtoto moja awe kiongozi, kiongozi anakaa katikati ya mduara ili kuwaona wanaokosea Msaidie kiongozi kuangalia atakae kosea (wanatakiwa kusimama kimya kama jibu ni hapana, na kuruka juu kama jibu ni nyama.

**Kiongozi:** nyama,nyama, nyama
**Wote:** nyama
**Kiongozi:** ya ng'ombe
**Wote :** nyama
**Kiongozi:** ya kuku,
**Wote :**nyama
**Kiongozi:** ya Simba
**Wote:** Kimya

**Warudie mara kadhaa ili waelewe vizuri mchezo.**



5) **Sema:** Tutabadili maneno na kutumia maneno yafuatayo.
6) **Sema:** Kiongozi utasema Chandarua , chandarua. Wengine waitikie chandarua, chandarua, chandarua na kuruka juu. Pale kiongozi atakapo taja kazi ambayo sio sahihi kwa chandarua, mkae kimya, msiruke juu wala kuiitikia chandarua.

   **Uliza:** kama wameelewa.
7) **Sema:** Sasa tunaaza mchezo kila mmoja akae tayari.
8) Hakikisha watoto wako kwenye mduara, wakumbushe masharti ni yale yale ya mchezo wa nyama, nyama, nyama. Wewe CCA ndio uwe kiongozi wa sehemu hii ya mchezo

**Kiongozi:** Chandarua! Chandarua!
**Wote:** chandarua!
**Kiongozi:** chandarua, chandarua!
**Wote:** chandarua
**Kiongozi:** kinazuia mbu
**Wote:** chandarua
**Kiongozi:** Kuvulia samaki
**Wote:** Kimya, wasiruke, watakao ruka wamekosea. Sema, chandarua kimetengenezwa kwaajili ya kujikinga na mbu wa malaria wakati wakulala. Sio kuvulia Kiongozi: Kinakukinga na malaria
**Kiongozi:** Kinakukinga na ugonjwa wa malaria
**Wote:** Chandarua
**Kiongozi :**hatari kwa afya
**Wote:** kimya, wasiruke, watakao ruka wamekosea,wametoka kwenye mchezo Waambie vyandarua vimedhibitishwa na Wizara ya Afya kuwa ni salama kwa afya ya watu wote hata watoto
**Kiongozi:** chandarua chandarua!
**Wote:** chandarua
**Kiongozi:** kinakupa usingizi mnono
**Wote:** Chandarua

9) Toa maelezo chandarua hakiumizi kifua kwa kuwa dawa iliyowekwa inaua mbu, haina madhara kwa watu.
10) Anaweza kuongeza matumizi mengine mabaya ya chandarua, imani potofu kuhusu usalama wa chandarua na faida za kulala kwenye chandarua
11) **Sema:** kwenye mchezo huu tulikua tunajifunza matumizi sahihi ya chandarua na usalama wa chandarua.

**Angalia walio baki kwenye mduara wapongeze kisha wapongeze wote kwa kushiriki zoezi hili.**

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Mkifika nyumbani waambie wazazi kuwa vyandarua vitumike kwa ajili ya kujikinga na mbu wa malaria tu, si vinginevyo. Watoto muwe mstari wa mbele kuelimisha jamii pale wanapotumia vyandarua vibaya. Zungumza na wazazi, waambie vyandarua vyenye dawa vimedhibitishwa kuwa ni salama kabisa kwa afya ya watu wote na watoto pia.

Sehemu ya 23:

# Mkutano wa Mama Seka

**Mama Seka anawaeleza wazee wenzake kwamba ni muhimu kwa wao kuwepo kwenye mkutano aliyouandaa ili kujadili jinsi gani jamii nzima inaweza kuungana ili kuitokomeza malaria hapo kijijini kwao. Zawadi anamuhaidi Bi Kiduku kuwa atakapo rudi kutoka shule atafanya usafi wa mazungira ya nyumbani kwani Mama Seka aliwaambia ni jukumu la lao kutunza afya yao.Mzee Limumi anamwambia Bi Kiduku awe anaenda kwenye mikutano ya pale kijijini.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Lengo la mkutano wa mama Seka lilikuwa ni nini?
   (***Jibu sahihi:*** Kujadili usafi wa mazingira wa hapo kijijini na kuhakikisha kwamba kila mtu analala kwenye chandarua kila siku)
2) Kwanini wanakijiji walikataa kuhudhuria mkutano wa Mama Seka?
   (***Jibu sahihi:*** Walisema wana kazi zao za kufanya)
3) Zawadi alikuwa anapeleka chepe la nini shule?
   (***Jibu sahihi:*** Kwenda kufanya usafi wa mazingira)
4) Kipindi cha patapata kimewafundisha nini watoto?
   (***Jibu sahihi:*** Kwamba ni muhimu kufanya usafi wa mazingira na kwamba ni jukumu lao wenyewe kutunza afya zao).
5) Zawadi aliahidi nini kwa Bi kiduku?
   (***Jibu sahihi:*** Kuwa wakimaliza kufanya usafi shuleni watakuja wafanye usafi nyumbani)

## Zoezi la 23: Kulala kwenye chandarua kila siku

**Waonyeshe watoto picha namba 9**


1) **Uliza:** Unaona nini kwenye picha **A**?
   (***Jibu sahihi:*** Watu wamelala kwenye chandarua).
2) **Uliza:** Ili kujikinga na ugonjwa wa malaria jamii inapaswa ifanye nini?
   (***Jibu sahihi:*** Kila mmoja inampasa alale kwenye ya chandarua kila siku)
3) Waonyeshe picha **B**:Uliza unaona nini katika picha B?
   (***Jibu sahihi:*** Baba na mama wanampeleka mtoto zahanati)
4) Unafikiri kwa nini huyu mtoto anapelekwa zahanati?
   (***Jibu sahihi:*** Kwasababu anaumwa)

**Sema:** kila mmoja kwenye jamii napaswa kuwajibika na afya yake.
**Unawajibika na afya yako kwa kufanya yafuatayo:**


- Hakikisha watu wote kwenye kaya yako wanalala kwenye chandarua kila siku kwa kipindi chote cha mwaka
- Wahi kituo cha afya mara tu uonapo dalili za ugonjwa wa malaria kwako au kwa mtu yoyote kwenye jamii yako.

Safisha mazingira ili kuharibu mazalia ya mbu. Usafi unafanyika kwa kuta vichaka na majani kuzunguka nyumba au shule na kuondoa vitu vinavyotunza maji aliyosimama kuzunguka nyumba na shule (mfano makopo, vifuu)

**A**



**B**




## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Waambie wazazi na marafiki zako ni wajibu wao kulinda afya zao kwa kuhakikisha wanalala kwenye chandarua chenye dawa kila usiku, wawahi kituo cha afya tu uonapo dalili za ugonjwa wa malaria na ni muhimu wasafishe mazingira ili kuharibu mazalia ya mbu.

**Agizo:** Wiki ijayo tutacheza mchezo wakuchora. Kila mmoja wenu aje kipande kikubwa cha karatasi na penseli yakuchorea

**Picha namba 9**





Sehemu ya 24:
# **Habari** Njema

**Bi Kiduku amekuwa mjasiriamali, anawashawishi wazee wenzake wanunue samaki kwa ajili ya familia yao kabla yakukaa kilabuni na kunywaa tu pombe. Mzee Boga anawapa habari njema wazee wenzake kuwa vyandarua vyenye dawa kama vile walivogaiwa watoto shuleni vinapatikana sehemu nyingine kwa malipo. Mzee Chanjagaa anafurahishwa sana na maendeleo ya Bi Kiduku na pia kumpa pongezi kwa kufuata ushauri kutoka kwa Zawadi.**

## Uliza maswali ili kupima uelewa

Baada ya kusikiliza kipindi, zima redio na uliza maswali yafuatayo ili kupima uelewa wa watoto juu ya kipindi.

1) Lengo la mkutano wa Mama Seka ulikuwa ni nini?
(***Jibu sahihi:*** Kujadili usafi wa mazingira wa hapo kijijini na kuhakikisha kwamba kila mtu analala ndani ya chandarua kila siku)
2) Bi Kiduku alikuwa anafanya biashara gani?
(***Jibu sahihi:*** Kuuza samaki)
3) Kwanini Mzee Boga alikataa kununua samaki wa Bi Kiduku?
(***Jibu sahihi:*** Kwa sababu hela aliyokuwa nayo alikuwa anaenda kununulia chandarua)
4) Ni njia gani zingine mtu anaweza kupata chandarua?
(***Jibu sahihi:*** Vyandarua vinapatikana pia maduka au kuptita hati punguzo)
5) Bi Kiduku alimwambia Mzee Chanjagaa nini siri ya mafanikio yake?
(***Jibu sahihi:*** Ni kuishi na kufuata ushauri wa Zawadi)

## Zoezi la 24: Upatikanaji wa chandarua

**Sema:** Zeozi la leo ni la kuchora. Kila mtu aandae karatasi na penseli yake au peni.

1) **Sema:** nitauliza swali, nyie mtajibu kwa kuchora.

**Mfano:** Nani anaeneza ugonjwa wa malaria? Jibu ni mbu, hivyo wanatakiwa kuchora picha ya mbu

2) **Sema:** Sasa zoezi linaanza,
3) **Uliza:** Mbali ya kugawiwa vyandarua shuleni, vyandarua vinaweza kupatikana wapi tena? (majibu yao yanaweza yakawa haya, madukani, kliniki ya wajawazito, n.k) hivyo watachora picha ya duka, na kliniki)
4) Baada ya kuchora, chagua washiriki wachache kama 2-3 waonyeshe michoro yao na waeleza, mfano mmoja kama amechora duka, atasema chandarua inapatikana dukani.
5) Na wengine wote warudie kusema kwa pamoja kuwa chandarua kinapatikana dukani kwa kununua.
6) **Uliza** kama kuna aliyechora hospitali, kliniki ya wajawazito au ofisi ya kata/kijiji, msaada wa mashirika ya dini. Wape nafasi waonyeshe picha zao.
7) **Sema**: nawapongeza kwa kuchora na kutoa majibu mazuri. Leo tunajifunza sehemu tunazoweza kupata chandarua mbali na kugawiwa shuleni. Kwa wale ambao hawata pata vyandarua shuleni wanaweza kupata chandarua kwa njia nyingine nyingi.


**Njia hizi ni:**

- Maduka kwenye jamii/vijiji vyetu yanauza vyandarua vyenye dawa
- Wajawazito wakienda kliniki wanapatiwa hati punguzo inayowawezesha kununua chandarua kw ash 500 tu
- Mashirika ya dini na kujitolea pia yanagawa vyandarua bure kwa baadhi ya watu.

8) **Uliza:** Nani mzazi, jirani au ndugu yake wamewahi kununua chandarua dukani? Angalia walionyoosha mikono, Halafu wapongeze!
9) **Sema:** Vyandarua vitagawiwa bure shule, lakini tunawajibu wakuongea na wazazi au walezi wetu kuhusu njia nyingine za kupata chandarua. Kama kuna mtu kwenye familia hana chandarua ni wajibu wazazi au walezi kununua chandarua dukani ili kuhakikisha kila mtu kwenye familia analala kwenye chandarua.

## Ujumbe wa kuhitimisha kipindi.

Wakirudi nyumbani waambie wazazi kuwa wawe tayari kununua vyandarua pale vile vya bure vitakapo koma. ili kuvunja mzunguko wa malaria.




# SIKILIZA PATAPATA

Kila jumamosi kwenye kipindi cha watoto

## Kupitia:

**Ruangwa FM** (Jumamosi saa 3 - 4 asubuhi) marudio Jumapili saa 12 jioni
**Safari FM** (Jumamosi saa 3 - 4 asubuhi) marudio Jumapili saa 2:40 asubuhi
**Pride FM** (Jumamosi saa 3 - 4 asubuhi) marudio Jumapili saa 10:15 jioni
**Jogoo FM** (Jumamosi saa 4 - 5 asubuhi) marudio Jumapili saa 5 asubuhi

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
CDC
President's Malaria Initiative
JOHNS HOPKINS BLOOMBERG SCHOOL of PUBLIC HEALTH
Center for Communication Programs
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii